ISD Powering solutions to extremism and polarisation

STRONG CITIES




# UUNDAJI NA UTEKELEZAJI WA KAZI-MIPANGO YA KUKINGA NA KUZUIA ITIKADI KALI ZA GHASIA KATIKA AFRIKA YA MASHARIKI

## CHOMBO CHA ZANA CHA STRONG CITIES CHENYE MAFUNZO KUTOKA KENYA


Patricia Crosby
Dominic Pkalya

# Kuhusu Chombo Hiki cha Zana

Chombo hiki cha zana kimeundwa na Strong Cities Network (SCN) kama rasilmali ya serikali za mitaa na mashirika ya kutetea haki katika Afrika ya Mashariki ambayo yana nia ya kuwa na kazi-mipango ya mitaani. Kazi-Mipango inanuia kujenga mtazamo wa sekta nyingi wa kuimarisha nguvu za jamii na kukabili vianzo vya itikadi kali za ghasia, uchochezi na chuki. Kwa makusudi ya chombo hiki cha zana, istilahi 'miji' inarejelea miundo yote ya serikali za mitaa kama vile kaunti, majimbo, mikoa au manispaa.

SCN inaunga mkono mameya, magavana, waunda sera na watendaji kazi kutumikia uelewa wao wa kimuktadha wa maeneo asilia katika uendelezaji wa kazi-mipango ya mitaani, kuchangia ushirikiano kati ya taifa na vijiji na utekelezaji wa uzuiaji uliojengeka kwenye misingi ya ushahidi na kuongozwa kutoka mashinani katika miradi imara inayotekelezwa kupitia miundo mbinu ya kinyumbani. Chombo hiki cha zana kinajengwa kutokana na tajiriba ya SCN katika utekelezaji wa mipango ya kinyumbani na uchangiaji wa uundaji wa kazi-mipango nchini Kenya, Jordan, Lebanon na Macedonia Kaskazini pamoja na utendaji bora wa kazi katika nyanja ya kimataifa kupitia kwa ushirikiano wa SCN na zaidi ya miji 145. Mifano ya ufanisi kimsingi inatokana na miradi iliyodhaminiwa na SCN nchini Kenya na kuchangiwa na mifano mingine ya ufanisi katika mipangilio ya kimataifa ya SCN. Chombo hiki cha zana kimefanikishwa kupitia kwa ushirikiano mpana na washirika wa kimaeneo, ikiwa pamoja na warsha ya washika dau 20 wa Kenya iliyofanyika mwezi wa Novemba 2020.

Mchakato wa Serikali ya Kenya wa Kukabili Itikadi Kali za Ghasia (NSCVE), uliochapishwa mwaka wa 2016, ulifungua njia ya ushirikiano thabiti wa kitaifa kuhusu masuala ya ulinzi ndani ya taifa la Kenya. Katika miaka minne iliyopita, mpango mahusi wa kinyumbani na mchakato unaongozwa katika kiwango cha kitaifa umeundwa. Safari hii ya sera haiwi rahisi, na utekelezaji unasalia kuwa na mianya, kama ambavyo chombo hiki cha zana kinaonyesha. Hata hivyo, licha ya changamoto za kila kukicha, kazi-mpango ya kaunti za Kenya (CAP) inafanya kazi kama kielelezo cha kufanyia kazi katika suala hili ibuka katika eneo la Afrika Mashariki na kuingiana na shughuli za kimataifa kuhusu Kazi-Mpango za Kinyumbani (LAPs).

Umuhimu wa kazi-mipango za kitaifa na kimaeneo ulitiliwa maanani na kukubaliwa kwa Kazi-Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Kuzuia Itikadi Kali ya Ghasia ambayo inapendekeza mtazamo wa ujumuishaji wa 'serikali-yote' na nyanja zote katika kupangia shughuli hii. Afisi ya Umoja Wa Mataifa ya Kukabili Ugaidi (UNOCT) kuhusu kupangia shughuli na mashirika mengine ya kimaeneo kama vile Tume ya Eneo la Ziwa Chad (LCBC) na Umoja wa Mataifa ya Ulaya (EU) yaliundwa.

*Kazi hii imepewa leseni na CC-BY 4.0 Leseni ya Kimataifa (https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/)*

Institute for Strategic Dialogue (ISD) ni kampuni ya kibiashara ya dhamana, anwani ya ofisi iliyosajiliwa S.L.P 75769, London, SW1P 9ER. ISD imesajiliwa Uingereza nambari ya usajili wa kampuni ni 06581421 na nambari ya usajili ya kutoa misaada ni 1141069.

# Shukrani

Kama inavyogharimu kijiji kumlea mwana – ama LAP – vivyo hivyo, inagharimu timu ili kuunda chombo cha zana. Shukrani kwa wenzetu katika Taasisi ya Mdahalo wa Mkakati (ISD) kwa ushauri, mchango na marekebisho - Daniel Hooton, Tim Hulse, Moustafa Ayad, Simeon Dukic, Besim Dogani and Veton Latifi. Tutakuwa tumekosea kama hatutawashukuru wenzetu kutoka katika mashirika wenza ambao wametusaidia katika usahihishaji wa kazi hii na kuongeza tajiriba zao, ili kuhakikisha kwamba chombo hiki cha zana kinatokana na mifano ya ulimwengu halisi na mafunzo kutokana nayo - Luqman Ahmed, Agnes Mwambila, Winnie Hachi, Bonventure Chengeck, Florence Osoo, Jonathan Rotino, Joseph Omondi, Walter Mwania na Shirley Otube.

Mwisho, tungependa kushukuru washirika wetu wote kutoka kwa serikali na mashirika ya kutetea haki kwa michango yao katika kuunda na kutekeleza Kazi Mipango ya Mitaani (LAPs). Utashi wenu, utaalamu wa kiufundi na kujitolea katika kujenga ustahimilivu wa kijamii ni kiungo kilichofanikisha kazi hii. Bila nyinyi, chombo hiki cha zana hakingewezekana kufanyika.

Asante kwa Kituo cha Kitaifa cha Kukabili Ugaidi (NCTC) Kenya, Serikali ya Kaunti ya Isiolo, Serikali ya Kaunti ya Kwale, Serikali ya Kaunti ya Lamu, Serikali ya Kaunti ya Nakuru, Serikali ya Kaunti ya Mombasa, Youth Bila Noma, Human Rights Agenda, Collaborative Women in Development, Isiolo Peace Link, Pastoralist Women for Livelihood and Social Support, Kikozi Programme Group, Kiunga Youth Bunge Initiative na Midrift Hurinet.

# Kuhusu Waandishi

**Patricia Crosby** ni Meneja wa Mipango katika ISD, akifanya kazi ya mipangilio yote ya SCN katika eneo la Afrika Mashariki. Alijiunga na ISD ili kuongoza upanuzi wa SCN katika Bara la Afrika na sasa anasaidia kaunti za Kenya ili kutekeleza CAPs zao kupitia kwa jitihada za kijamii za Multi-Year PROACT. Patricia anawajibikia uundaji wa ala za mafunzo, kusaidia katika kukuza ushirikiaano kati ya serikali kuu na mitaa na kutoa msaada wa moja kwa moja wa sera na mipangilio kwa mashirika ya kijamii na wadau wa serikali. Kabla ya hapa, Patricia alifanya kazi na Jumuiya ya Commonwealth katika kitengo cha Kukabili Itikadi Kali za Ghasia, kuunda na kutekeleza miradi ya serikali ya kujenga uwezo wa watu. Patricia pia amefanya kazi na serikali ya Canada, hasa kushughulikia migogoro, dharura za kibalozi na mipangilio ya maendeleo ya Mashariki ya Kati. Patricia alihitimu kutoka Chuo Kikuu cha Ottawa na Shahada ya Sayansi ya Kijamii katika Maendeleo ya Kimataifa na Utandawazi.

**Dominic Pkalya** ni Meneja Mkuu wa Eneo katika ISD, akifanya kazi katika michakato yote ya ISD ya kukabili ugaidi nchini Kenya na eneo pana la Afrika Mashariki. Dominic pia anasaidia katika uundaji wa sera, utafiti, mafunzo na mbinu za ufuatiliaji na tathmini ili kupima athari za mipango ya kukabili ugaidi ndani na nje ya mitandao. Dominic anasimamia mipangilio ya kijamii ya PROACT ya kuingilia kati pamoja na kusaidia kazi za SCN na Young Cities nchini Kenya. Hapo mbeleni Dominic alikuwa msimamizi wa muradi unaodhaminiwa na USAID, unaoshughulikia uimarishaji wa nguvu za kijamii ili kukabili misimamo mikali katika eneo la pwani ya Kenya. Aliwahi kufanya kazi na Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP) Kenya, akiwa ametumwa kwa Mamlaka ya Kuzuia Ukame, akitoa msaada wa kiufundi wa kupunguza ghasia zinazotokana na silaha baina ya jamii za wafugaji nchini Kenya. Ana shahada ya uzamili katika Uanahabari, Mizozo na Masomo ya Amani kutoka katika Chuo Kikuu cha Umoja wa Kimataifa cha Amani na Shahada ya Sanaa katika masuala ya Serikali na Utawala wa Umma kutoka Chuo Kikuu cha Moi, Kenya.

# Yaliyomo

## Sura 1 — Utangulizi wa Chombo cha Zana

1.1 Kwa nini miji? 5
1.2 Muhtasari wa chombo cha zana 7

## Sura 2 — Kuelewa LAPs

2.1 SCN 9
2.2 Mchakato wa kuunda na kutekeleza LAP 11
2.3 Kanuni zinazoongoza LAPs 12
2.4 Kielelezo cha CAP cha Kenya 13

## Sura 3 — Kuanza & Kutunga LAP

3.1 Bainisha sababu ya kuwepo na LAP 17
3.2 Tunga LAP 21

## Sura 4 — Kutekeleza LAP

4.1 Kuzindua na kuwasilisha ujumbe wa LAP 28
4.2 Kuhakikisha LAP inafanya kazi 30
4.3 Kufadhili LAP 31
4.4 Kusahihisha na kurekebisha LAP 34

## Sura 5 — Ufuatiliaji & Tathmini LAP

5.1 Kuanzisha ToC 36
5.2 Kuunda viashiria 40
5.3 Kukusanya deta za kupima kufaulu 43

## Viambatisho —

Kiambatisho A - Faharasa 45
Kiambatisho B – Aina tatu za kanuni za kuongoza 48
Kiambatisho C – Orodha ya kukagua uundaji wa LAP 51
Kiambatisho D – Kiwiliwili cha LAP 55
Kiambatisho E – Kiolezo cha kazi mpango ya mwaka 57
Kiambatisho E – Kiolezo cha ToC 58
Kiambatisho G – Kiolezo cha jedwali la kiashiria cha kufuatilia 59

Makala ya tamati 60

# Sura ya Kwanza
## Utangulizi wa Chombo cha Zana

### 1.1 Kwa nini miji?

Kufikia mwaka wa 2050, 68% ya watu duniani watakuwa wakiishi mijini[1] na wataathirika na mchanganyiko wa vitisho. Kutoka kwa ghasia za kisiasa na mashambulizi ya kigaidi ya kimataifa hadi ongezeko la uhalifu wa chuki na kupotoshwa mtandaoni, changamoto za leo ni za kipaumbele cha kidunia na zenye uhalisia wa kinyumbani.
Serikali za kitaifa zimejaza ajenda za kiusalama, na kuzuia/kukabili itikadi kali za ghasia (P/CVE) na mara nyingi mikakati imepuuza umuhimu wa serikali za mitaa. Hata hivyo, miji[2] are uniquely placed to facilitate, galvanise and connect to community leaders through a number of vantage points, including the following:

- ***Viongozi wa mitaa wanajua jamii zao vizuri na kwa hivyo wana uwezo wa kushirikisha shughuli vyema. Kwa kushirikisha kazi hii, wanakuwa na athari kubwa kwa maendeleo ya baadaye ya jamii zao.***

- ***Viongozi wa mitaa na washikadau huenda wakawa na imani ya wananchi wao kwa sababu ya kwamba wanaishi karibu. Imani hii ni muhimu katika kuaminika na athari ya jititahada za kinyumbani za kuzuia, jambo ambalo linakosekana katika taasisi za juu au katika kiwango cha kitaifa.***

- ***Inajulikana kuwa wengi wa wanaoendesha mafunzo ya misimamo mikali wanapatikana miongoni mwa wananchi,[3] ikuonyesha umuhimu wa kuwa na juhudi ya kuzuia karibu na wananchi [4]***

- ***Hali za kiusalama zinazodhoofika zinakuwa na athari wakati wa kupiga kura, hivyo basi kufanya viongozi wa mitaa kuzuka na ajenda za kuzuia na kudhihirisha umilisi.***

- ***Serikali za mitaa zina uwezo wa kuitisha mikutano na kushirikisha huduma za kinyumbani zinazotolewa kirasmi ama kwa njia zisizokuwa rasmi, ambazo zinaweza kutolewa kando kando japo zinalenga jamii moja. Hizi zinaweza kuwa pamoja na huduma za kijamii, elimu, matibabu na mipango ya vijana.***

Yaliyomo —

## Kwa nini LAPs?

Kwa kuunda LAPs, serikali za mitaa zitakuwa daraja kati ya mikakati ya serikali kuu na watu walio katika msitari wa mbele katika kukabiliana na changamoto mashinani. Huku serikali kuu ikiongoza mikakati ya kitaifa ya P/CVE na kufanya rasmi sera husika, serikali za mitaa zimo katika nafasi nzuri kutambua hatari za pale kwao, kujenga ushirikiano na kuunda jitihada faafu za kuzuia.[5] LAPs inasaidia kujenga ushirikiano wa kiwango cha kitaifa na mtaa kwa kuunda malengo, vipaumbele, rasilamali hitajika, ushirikiano muhimu na makataa ya kiuhalisia kwa utekelezaji mwafaka.
LAPs inatoa fursa kwa jamii kuunda mtazamo wa ustahimilivu kwa misingi ya kutoka chini kwenda juu, kuhahakikisha mbinu ya umoja na mtazamo wa ushirikiano na uelewa wa pamoja baina ya wadau wa mtaa kuhusu masuala muhimu na majukumu ya kila mmoja. Hii inasaidia kuepuka dosari za mikakati ya kitaifa, ambayo inaweza kutokana na ukopaji na upachikaji bila kuiambatanisha na miktadha mwafaka ama tofauti kati ya hoja sababishi za misimamo mikali ya ghasia kutoka sehemu moja hadi nyingine.[6] Muhimu ni kuwa, ina ruhusu jamii za mitaa kuunda majibu ambayo ni tofauti na yale ya mdahalo na mwelekeo wa kisiasa wa kitaifa.

Kupitia kwa LAPs, serikali za mitaa zinaweza kutumia uwezo wao wa kuitisha mikutano na kujumuisha shughuli za P/CVE katika mipango mipana ya maendeleo na kukumbatia mtazamo wa 'mji-mzima.' Kwa kujumuisha jitihada za ustahimilivu katika njia kama vile elimu au mitaa kujilinda, miji ina uwezo wa kutafuta rasilmali za kushughulikia shida za miundo ambazo huenda zikasababisha uchochezi na misimamo mikali.

### *Historia ya Kazi-Mpango katika Afrika ya Mashariki*

*Kuna sera kadhaa za maendeleo zilizoundwa na Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika na nchi ambazo zimepelekea serikali za mitaa katika Afrika Mashariki kuunda LAPs zao katika miaka ya hivi punde. Hata hivyo, ni muhimu kuelewa kuwa P/CVE na jitihada za kukabili ugaidi sio mpya katika bara hili. Kilicho kigeni, hata hivyo ni kutambua kwamba serikali za mitaa zinatekeleza wajibu muhimu katika kukabiliana na changamoto hizi. Baadhi ya hatua muhimu ni pamoja na:*

- ***1999*** *Mkutano wa Umoja wa nchi huru za Afrika kuhusu Kuzuia na Kukabili Ugaidi*
- ***2002*** *Kazi Mpango ya Umoja wa Afrika kuhusu Kuzuia na Kukabili Ugaidi*
- ***2006*** *Mkakati wa Umoja wa Mataifa wa Kujibu Ugaidi na mihimili ambayo bado inaongoza kazi mipango*
- ***2010*** *Mwakilishi Maalum wa Ushirikiano katika kujibu Ugaidi.*
- ***2011*** *Sheria Kielelezo ya Kuzuia Ugaidi*
- ***2015*** *Malengo ya Mandeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa*
- ***2016*** *Kazi Mpango ya PVE ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa*
- ***2017*** *LAP ya Kwanza Barani Afrika kuzinduliwa katika Kaunti ya Kwale, Kenya.*

Yaliyomo —

## 1.2 Muhtatasari wa Chombo cha Zana

Chombo hiki cha zana kinanuia kujaza pengo la rasilamli za sasa zilizoko kwa serikali za mitaa na washikadau wa mashirika ya kupigania haki ambao wangependa kuunda na kutekeleza LAP. LAP itafanya kazi kama jukwaa kwa miji kuunda majibu yao kwa misimamo mikali, uchochezi na chuki kwa mujibu wa muktadha. Pamoja na kwamba miswada mingi kuhusu juhudi za P/CVE ziko katika kiwango cha mtaa, inapungukiwa na uwezo wa kuongoza serikali za mitaa katika uundaji wa majibu tekelezi kupitia kwa LAPs. Chombo hiki cha zana kinaangazia suala hili la kazi mpango kwa mtazamo mpya, kwa kutumia mifano halisi ya ulimwengu na mazoezi ibuka kutoka Afrika Mashariki na jamii ya kimataifa ya SCN ili kuonyesha kuwa suluhu za kinyumbani zinaweza kupatikana kwa changamoto za kinyumbani.

Serikali za mitaa pamoja na washikadau wa mashirika ya kutetea haki wako katika nafasi bora kukabiliana na masuala ya mitaa, lakini mara nyingi hukosa rasilmali na uwezo wa kiufundi kufanya hivyo. Chombo hiki cha zana kinadhihirisha namna ambavyo inawezekana kuunda na kutekeleza LAP kutokana na rasilmali kidogo za kifedha au bila. Kwa mtazamo mpya wa uendelevu nje ya misaada ya wafadhili, chombo hiki cha zana kinapania kumotisha washirika wa mitaani kusababisha na kukumbatia mabadiliko chanya.

### Jinsi ya kutumia chombo hiki cha zana

Chombo hiki cha zana kinajumuisha sura tano na faharasa ya istilahi muhimu na nakala sita za mazoezi. Sura ya kwanza na ya pili ni za kutanguliza chombo cha zana na kazi mpango. Sura ya tatu na ya nne zinatoa hatua za kutunga na kutekeleza LAP. Sura ya tano inatoa maelezo ya ushauri ya kuunda misingi ya ufuatiliaji na tathmini ya LAP. Kila sura ina matarajio ya mafunzo katika kisanduku cha rangi ya kizambarau mwanzoni.

**Baada ya kusoma sura hii, hakikisha kuwa unaelewa:**

1. Umuhimu wa kupata uungwaji mkono kutoka kwa wanasiasa
2. Mchakato wa kuchanganua hatari
3. Namna ya kuainisha majukumu na wajibu wa jopo kazi lako la muda.
4. Hatua tano muhimu za kutunga LAP.

Katika chombo kizima cha zana, maswali muhimu yameainishwa katika herufi za italiki katika kisanduku cha rangi ya samawati katika anwani zenye rangi ya samawati.

***Na je ikitokea kuwa serikali yangu ya mtaa sio mji?***

*SCN inafanya kazi na serikali zote za ukubwa wa aina zote, ikiwa pamoja na kaunti, mikoa, majimbo na manispaa. Chombo hiki cha zana kinatumia maneno 'mji' na 'serikali za mitaa' kwa kubadilishana kurejelea aina zote miundo ya serikali ndogo.*

Yaliyomo —

## 1.2 Muhtatasari wa Chombo cha Zana

Mifano ya mipangilio ya SCN pia imo katika visanduku vyenye rangi ya samawati lakini anwani zake zimekolezwa.

***Mfano: Kikundi Kazi cha Jamii ya Kumanovo***

*SCN ilisaidia manispaa ya Kumanovo kuanzisha shirika linalojumuisha sekta nyingi – Kikundi Kazi cha Kijamii (CAT) – ili kutunga na kutekeleza sera na mpangilio wa P/CVE. Kwa kufanya kazi na taasisi zilizoko, CAT iliundwa kirasmi kwa amri ndani ya Baraza la Uzuiaji la Mtaa, kitengo kinachoshughulika na masuala yote yanoyohusiana na uzuiaji katika manispaa, kama kikundi cha kudumu chenye jukumu la kutunga na kutekeleza kazi mpango ya P/CVE katika mtaa. Amri inayounda CAT inataja taasisi zinazojumuishwa katika kazi yake na zinatarajiwa kutuma mwakilishi. Jambo hili linahakikisha kuwa washikadau wote muhimu na utaalamu wao wanajumuishwa wakati wa kutunga sera za mtaa kwa njia ya kuwajibisha. Pindi stakbadhi ya sera ilipoundwa, wanachama wa CAT waliiwasilisha katika Baraza la Mtaa la Uzuiaji ambapo ilikubalika kwa amri. Taratibu hizi zinahakikisha kuwa kazi hii inatiwa katika mfumo na tasisi, matokeo yake yakiwa kukubalika, kuwajibika na kuendelezwa kwa kazi inayohitajika kutekelezwa kutokana na LAP.*

Mifano kutoka nyanjani, ambayo kimsingi ni mafunzo kutokana na utekelezaji wa CAPs nchini Kenya, iko katika herufi za italiki katika visanduku kwenye rangi ya machungwa na taa za rangi ya mchungwa.

*Kaunti nyingi za Kenya zimedhihirisha utekelezaji kwa kuunda wasimamizi wa mihimili. Nchini Kenya, kazi za CAP zinapanga maudhui makuu kama vile 'elimu,' 'itikadi' na 'uchumi.' Wasimamizi wakuu wana wajibu wa kushirikisha kazi na kufuatilia maendeleo katika sehemu zao za kipaumbele. Hii inafaulisha sio tu kushirikisha kazi bali pia uwezo wa washikadau kupima ufanisi wa CAP.*

# Sura ya Pili

## Kuelewa LAPs

Sura hii inatoa msingi wa ushirikishwaji wa vitengo mbalimbali katika kiwango cha mtaa. Inaangazia mtazamo wa SCN, mafungu matatu ya zile kanuni za mwongozo na kielelezo cha Kenya cha CAP.

**Baada ya kusoma sura hii, hakikisha kuwa unaelewa:**

1. Kilicho muhimu katika mtazamo wa SCN na kinachojumuishwa katika kielelezo cha mji cha SCN.
2. Mchakato ambao miji inafaa kufuata katika uundaji na utekelezaji wa LAPs.
3. Mafungu matatu ya kanuni za mwongozo na umuhimu wake katika uundaji na utekelezaji wa LAPs.
4. NSCVE na vizazi vitatu vya CAPs.

***Itakuwaje iwapo serikali yangu ya mtaa sio mji?***

*SCN inafanya kazi na serikali zote ndogo zenye ukubwa tofauti tofauti, ikiwa pamoja na kaunti, majimbo na manispaa. Chombo hiki cha zana kinatumia istilahi 'mji' na 'serikali ya mtaa' kwa kubadilisana kurejelea aina zote za miundo ya serkali ndogo.*

## 2.1 SCN

SCN ilizinduliwa katika mwaka wa 2015 kwenye Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa ili kuanzisha majibu yanayoongozwa na miji dhidi ya aina zote za chuki, uchochezi na misimamo mikali. Tunauliza wanachama wetu kushirikiana na mitaa yao kuunda na kutumia majibu ya mitaa kwa changamoto zenye utata, kuhakikisha kuwa hakuna mji unaokabiliana na vitisho hivi peke yake.

Kupitia kwa **mikutano ya kimataifa** ya SCN, **kubadilshana mawazo miongoni mwa miji** na **warsha za kimaeneo**, wanachama wetu wanajenga madaraja, wanajadiliana kuhusu sera bunifu na kubadilishana mazoezi mema na wenzao kutoka kwa wataalamu kutoka kwa miji mikubwa ya kimataifa. SCN inatoa **vielelezo vya kujenga uwezo, uingiliaji kati na mazungumzo miongoni mwa vijana** kwa njia nyingi na kwa kindani. Zana za SCN na vielelezo vya kisera vinatumika kote duniani, kutoka Australia hadi Macedonia Kaskazini, Lebanon hadi Marekani, na Kenya hadi Uingereza.

**SCN Five Work Stream Pillars**

| Kubuni: Sera na Mkakati | Kujenga: Miundo mbinu ya Mtaa ya Kuzuia | Mafunzo: Kufunza na kukuza uwezo wa watu | Kupasha: Deta & Zana | Kuunganika: Ushirikiano wa kimataifa na kimtaa |
|---|---|---|---|---|

## Mbinu yetu

Ingawa serikali za mitaa ni tofauti kwa mujibu wa ukubwa, uwezo na hatari zinazopitia, tunaaamini kuwa kuna kanuni kuu na matokeo ambayo ni sharti miji kuwa nayo kama ushahidi wa juhudi zao za P/CVE.

| Kanuni Muhimu za SCN kwa LAPs | Matokeo ya SCN yanayotarajiwa kwa LAPs |
|---|---|
| **Mji-mzima:** Mtazamo kamilifu wa sekta nyingi. | **Kukadiria hatari inayopatikana mtaani:** Stakbadhi hai inayoonyesha tatizo katika muktadha na kutambua uzuri, unyonge, fursa na vitisho. |
| **Kutaarifu kwa deta:** Taarifa inatokana na deta na ushahidi. | **LAP:** Mbinu au mkakati unaoonyesha mbinu ya serikali ya mtaa kwa P/CVE ikiwa na malengo na matokeo yaliyo wazi. |
| **Mtaa kuongoza:** Imeundwa na kuongozwa na jamii huku serikali ya mtaa ikifanya kazi ya ushirikishaji. | **LPN:** Shirika linaloshirikisha sekta nyingi (mtandao wa mtaa wa kuzuia) linalohakikisha utekelezaji wa LAP. |
| **Uendelevu:** Umejumuishwa ndani ya miundo na makadirio ya fedha iliopo pale panapowezekana. | **Kiongozi mshirikishi wa Kuzuia:** Kituo kilichotengwa kinachoshirikisha juhudi za P/CVE (kitahitajika tu iwapo makadirio ya fedha yanaruhusu na kiwango cha hatari kikiwa juu) |
| **Ushirikiano wa taifa na mitaa:** Kuungwa mkono na wadau wa kiwango cha kitaifa kupitia mawasiliano ya mara kwa mara kwa njia zote mbili. | |

***Ni nini maana ya mji kielelezo wa SCN?***

*Kielelezo cha mji wa SCN kinajumuisha sekta nyingi na kinalenga mtaa kwa LPN unaongozwa na mshirikishi wa kuzuia, uendelevu kuhusishwa katika mikakati ya kijiji na ya kitaifa, ukiongozwa na LAP na kutaarifu kutokana na ushahidi wa kukadiria hatari.*

## 2.2 Mchakato wa kuunda na kutekeleza LAP

***Mji wangu unahitaji kazi mpango ya mtaa?***


*Ni rahisi kuchukulia kuwa miji yote lazima iunde LAP na kwamba ni lazima iangazie tu P/CVE. Hata hivyo, miji huwa tofauti katika hatari zao na masuala nyeti. Miji yote inakabiliana na changamoto nyingi, kutoka kwa makazi na masuala ya mazingira hadi kwa uhalifu na ghasia. Miji mingi haina fedha za kutosha ili kukabiliana na changamoto hizi, na kuna tofauti kubwa ya kazi za miji hii. Kwa hivyo, hatupendekezi kuwa miji yote inakumbatia P/CVE LAPs, lakini tunapendekeza kwamba miji yote ifanye ukadiriajii wa hatari, ambao utaonyesha kama kazi mpango inahitajika kuundwa.*

**Anzisha:** Miji yote sharti kwanza ihakikishe mkakati wa kuungwa mkono kwa LAP na wanasiasa katika kiwango kinachofaa cha serikali kisha ikadirie hatari ili kuelewa hatari ambayo mji ama eneo linakabiliana nayo. Iwapo kiwango cha hatari kiko juu, hivyo LAP inahitajika na jopo kazi la muda linahitajika kuundwa ili kuongoza mchakato.

**Unda:** Iwapo tathmini ya awali ya hatari iko juu, mji lazima uunde LAP ambayo: inataarifishwa na deta na ushahidi, ina lengo na matokeo ya kupimika, inaongozwa na jamii, ina miundo wazi ya ushirikishwaji, na imejumuishwa katika sheria ya mtaa ama miundo ya kisera.

**Tekeleza:** Iwapo mji una LAP, sharti mji utekeleze LAP kwa: kufanya hafla ya uzinduzi na kuzungumzia yaliyomo kwa jamii, kuanzisha sera zinazoisaidia, kutengeneza kazi mpango ya kila mwaka inayofadhiliwa kwa kutumia rasilmali zilizoko, kutumia makadirio na fedha za kitaifa na za mtaa, kuzungumza na sekta za kibafsi, na kufikia fedha za wafadhili.

**Fuatilia:** Miji yote iliyo na LAP sharti kila mwaka itathmini athari na kutengeneza kazi mpango ya kila mwaka, na kusahihisha miundo ya ushirikishaji ili kuongeza au kuondoa mashirika au mahali pao pa kutagusana. Miji yote isiyokuwa na LAP lazima isahihishe na kuangalia upya tathmini ya hatari.



## 2.3 Kanuni zinazoongoza LAPs

LAP zote sharti zijengeke kwenye kanuni zinazoonyesha uhalisia wa kimtaa na wa kitaifa, kwa mwongozo wa kieneo na kimataifa. Pale ambapo pana mikakati ya kitaifa, LAP sharti ionyeshe hizi stabadhi ili kuhakikisha kuwepo kwa ushirikiano wa kitaifa na kimtaa. Kanuni zinazoongoza zinaweza kugawanywa katika makundi mtatau:

1. **Kukumbatia vigezo** vinavyoonyesha umuhimu wa mkakati na njia ya LAP.
2. **Masharti ya mchakato na uongozi** ambayo yanadhihirisha mbinu za kutunga LAP na muundo wa ushirikishaji.
3. **Sehemu za kipaumbele** zinazobainisha makundi makuu ya maudhui ya kuingilia kati.

Serikali za nchi zingine zimeainisha kirasmi kanuni zinazowaongoza – kama vile Serikali ya Kenya katika NSCVE na mwongozo wa kuunda CAPs. LCBC iko na mfano wa kimaeneo katika Mkakati wa Kimaeneo wa Kusawazisha. Katika kiwango cha kimataifa, UNOCT imechapisha mwongozo wa kurejelewa katika uundaji wa kazi mipango ya kitaifa na kieneo. Makundi haya matatu ya kanuni za miongozo yanapatikana katika Kiambatisho B.

### Vigezo vya kukumbatia

Kabla ya kuunda LAP, serikali za mitaa zinafaa kuamua vigezo vya kukumbatia vinavyotambua umuhimu na kuongoza LAP yao. Hakikisha kuwa masharti ya kukumbatia yanaonyesha muktadha wa mtaa na mahitaji ya mji wako. Vigezo vya kukumbatia vinaweza kuwekwa katika kategoaria zifuatazo:


- **Uwajibikaji, uongozi na uwazi:** Umedumisha mchango wa kisiasa na umilikaji katika kiwango faafu, unaotambua wajibu wa wahusika wa kitaifa, kieneo na/au kimatifa.
- **Ushirikishaji:** Unainisha jinsi ambavyo wahusika wataweza kuwa wabunifu na wenye kuathiri na kuanzisha ushirikiano unaojenga mahusiano thabiti yenye kunufaisha pande zote mbili.
- **Mbinu:** Inadhihirisha kuwa mbinu zinasheheni ushahidi, kujengwa kwa misingi ya ufahamu wa kimtaani, yenye sekta nyingi na jumuishi; na zinaheshimu ala za haki za binadamu, jinsia na mtazamo wa kutodhuru.
- **Zana:** Inabainisha masharti faafu au zana zinazohitajika katika utekelezaji.
- **Matokeo:** Inataja matokeo yanayotarajiwa, kwa mfano: 'uwezekano uliopunguzwa wa kusajiliwa na kufanywa mtu wa itikadi kali' au 'inachangia Malengo ya Mendeleo Endelevu.'

## Masharti ya Mchakato na Uongozi

Ni sharti LAPs ziandikwe na kuongozwa katika njia inayoheshimu masharti na ushauri wa kitaifa, kieneo na/au kimataifa. Mwongozo wa kurejelewa wa UNOCT unatoa kanuni sita za kufuatwa kwa mchakato wa hatua kwa hatua ili kuhakikisha kuwa mipango ya P/CVE inatekelezeka, ni pana na jumuishi. Huku stakbadhi au sera nyingi za serikali zikitaja kwa ufinyu kazi ya LAPs, NCTC ya Kenya imefafanua sheria 12 ili kuongoza na kushirikisha CAPs. Tazama Kiambatisho B kupata orodha kamili.

## Maeneo ya kipaumbele

Pamoja na kanuni zinazoongoza, LAPs zinafaa kuongozwa kupitia mihimili ya maudhui ili kuweka pamoja makundi ya majibu. Mihimili inafaa kuwakilisha mtazamo wa ujumla wa mji-mzima badala ya mtazamo mfinyu wa usalama. Ni muhimu kutaja kuwa kidogo huwa kikubwa ikija kwenye mihimili. Ili LAPs ifanye kazi, kuorodhesha vitendo vyenye uhalisia na kuafikika ni mihimu.




## 2.4 Kielelezo cha CAP cha Kenya

### Usuli wa Vitisho Nchini Kenya

Ushambulizi wa bomu wa Ubalozi wa Marekani na al-Qaeda mjini Nairobi, nchini Kenya mwaka wa 1998, ulioua watu 224, ulianzisha kipindi kipya cha itikadi kali za ghasia ambacho kimegusa sehemu zote za jamii ya Kenya. Japo shambulizi hili kiasilia lilikuwa la kiislamu, lilikuwa sehemu ya ghasia za kikabila ambazo hufadhiliwa na wanasisa, kilele chao huwa katika misimu ya uchagaguzi. Leo hii katika Kenya, vitisho vya al-Shabab vimepiku hivi vingine, ambavyo katika siku za hivi karibuni, vimeongezeka katika jitihada za usajili katika maeneo yote ya Kenya. Usajili huu umetiwa nguvu na athari kutoka kwa Taifa la Kislamu la Irag na Syria (ISIS), ambalo mbinu zake za propaganda zimefanikiwa katika kuvutia wapiganaji wa kigeni kutoka pembe zote za dunia.

***Vivutio Vikuu Vya Misimamo Mikali Nchini Kenya:***

- *Mitazamo ama ya kweli au ya kufikirika ya kutengwa kisiasa na serikali za baada ya uhuru kwa maeneo yanayokaliwa kwa wingi na waislamu.*
- *Ugumu wa jamii hizi wa kupata stakbadhi kama vile pasipoti na hati za kumiliki mali.*
- *Kiwango cha juu cha kukosa ajira miongoni mwa vijana.*
- *Serikali (vyombo vya usalama) kupita mipaka katika operesheni za kukabiliana na ugaidi.*
- *Kwa njia ya jumla kuainisha jamii za kiislamu kama zinazokubali, kusaidia ama kuvumilia ugaidi.*

Yaliyomo —

- **2011** — Oparesheni ya Linda Nchi
- **2012** — Sheria ya Kuzuia Ugaidi (POTA)
- **2014** — Uundaji wa Kitengo cha Polisi cha Kitaifa cha Kupambana na Ugaidi (ATPU)
- **2016** — Mkakati wa Kitaifa wa Kukabiliana na Misimamo Mikali ya Ghasia (NSCVE)
- **2017** — Kizazi cha Kwanza cha CAPs
- **2018** — Kizazi cha Pili cha CAPs
- **2019** — CAPs za Kasi na Marekebisho ya POTA

## Juhudi za Serikali ya Kenya za Kupunguza Athari

Kama njia ya kukabili vitisho vya kiwango cha juu vya itikadi kali za ghasia (VE), Serikali ya Kenya ilianzisha msururu wa mbinu za P/CVE. Hatimaye mbinu hizi ziliwezesha kuanzishwa kwa CAPs za P/CVE. Kenya ni moja kati ya nchi pekee duniani ambazo ziko na LAPs za kitaifa zinazotambuliwa na serikali na kuhusisha mbinu na miundo katika ushikishwaji.

## Vizazi vitatu vya CAPs

Kaunti 47 za Kenya zinakabiliwa na mazingira na changamoto nyingi tofauti. Zaidi ya hayo, mchakato wa Kenya wa ugatuzi ni moja kati michakato yenye matarajio makubwa zaidi duniani. Ugatuzi unatoa njia ya kukabiliana na changamoto za mtaani kwa njia bora zaidi na ni katika muktadha huu ndipo NCTC iliona nafasi ya kuanzisha CAPs. CAPs zimepitia viwango vingi na zinaweza kugawanywa katika vizazi vitatu:

- ***Kizazi cha Kwanza cha CAPs*** *Zilikuwa stakbadhi za miaka mitano ya mikakati ya maendeleo katika eneo la pwani, ambalo lilikuwa linashambuliwa sana wakati huo. Hili lilikuwa jaribio la kwanza la kufanya P/CVE kuwa kazi inayowajibikiwa kwa pamoja na mchakato wa papo hapo uliongozwa na mashirika ya kijamii.*

- ***Kizazi cha pili cha CAPs*** *Eneo la pwani lililosalia, Kaskazini Mashariki na Upembe wa juu wa kaunti za Mashariki zilifuata mchakato wa maendeleo ulioidhinishwa na NCTC na kuchota kwa kiasi kikubwa kutoka kwa mihimili ya maudhui ya NSCVE na kufanywa wa nyumbani. Kulikuwa na juhudi kubwa za kuboresha utafiti na upimaji na tathmini ya kazi na kuanzisha mchakato wa kushauriana uliosababisha kuanzishwa kwa Ukumbi wa Mashauriano baina ya Kaunti (CEFs).*


- ***Kizazi cha tatu cha CAPs, ama CAPs za Kasi (RCAPs)*** *Stakbadhi fupi za mwaka mmoja kwa kaunti zote zilizosalia. RCAPs zote ziliundwa katika warsha za siku moja au mbili na kwa hivyo zikakosa utafifiti na mchakato wa ushauriano ambao vizazi vya awali vilinufaika nao. Waliendeleza CEFs na kuhimiza kuanzishwa kwa CEFs ndogo.*

## Muundo wa kielelezo cha CAP

Kenya iko na mfumo shupavu wa kuongoza mkakati na sera pamoja na utekelezwaji wa miradi ya P/CVE. Kama ilivyoonyeshwa katika mchoro wa hapa chini, kazi ya P/CVE inaendeshwa katika kiwango cha kitaifa na NCTC, ambayo inawajibika moja kwa moja kwa rais. Mkakati wa P/CVE katika kiwango cha kitaifa unaongozwa na NSCVE iliyochapishwa katika mwaka wa 2016. Mkakati mpya umeundwa kwa miaka mingi na unatarajiwa kuzinduliwa hivi karibuni.

Kila moja ya kaunti 47 ina CAP na CEF. CEF ni shirika lililo na wajibu wa utekelezwaji wa CAP, na lina uenyekiti wa pamoja kati ya Kamishna wa Kaunti na Gavana. Inajumuisha washikadau kadhaa wa serikali na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali. Kauti zingine pia zina CEFs za kaunti ndogo au makundi tendakazi ya mihimili ya maudhui.

Hata kama sio stakbadhi ya P/CVE, Mipango Shirikishi ya Maendeleo ya Kaunti (CIDPs) na bajeti za kaunti ni muhimu katika utekelezwaji wa CAP kwa vile inatoa njia ya kuzijumuisha kazi za CAP katika mikakati iliyo na rasilmali za kifedha.




## Mafunzo kutoka kwa kielelezo cha CAP cha Kenya

Ingawa kielelezo cha CAP cha Kenya kimepongezwa kama ishara ya ufanisi katika mipangilio ya mtaa ya uzuiaji, utekelezwaji umekumbwa na changamoto nyingi. Mafunzo kutokana na changamoto hizi yanaweza kusaidia serikali za eneo zima katika kuunda michakato ya LAP zao.

Ushiriki wa jamii za mitaa, mashirika ya kijamii ya mashinani na wasomi hufanikisha ukubalifu wa CAPs. CAPs katika eneo la pwani yaliongozwa na wasomi kutoka katika kaunti za pwani. Hili liliimarisha ukubalifu wa CAPs na jamii za kule.[7]

> ***Funzo:*** *LAP yafaa kuhakikisha kuwa siku zote watu kutoka jamii ambapo itatumikiwa wanahusishwa kikamilifu katika utafiti na kutunga LAP. Washikadau wa mtaani wanafaa kuhusisha tu wataalamu kutoka nje wakati kuna pengo la kitaalamu na iwe tu katika majukumu ya ushauri ama kutoa uwezo wa kitaalamu kwa wasomi wa pale na wadau wengie.*

CAPs zinanuiwa kuwa jukumu la pamoja kati ya serikali ya mtaa na serikali kuu. Hata hivyo, kwa vile maendeleo yao yameongozwa na wawakilishi wa serikali kuu, nyingi ya serikali za mitaa hazihisi kuhusishwa, jambo linaloleta kutotaka kufadhili shughuli ama kujumuishwa na shughuli za kaunti kama vile CIDPs.[8]

***Funzo:*** *Ni muhimu kuwa na usawazishaji kati ya uhusishwaji wa serikali ya mtaa na ile ya serikali kuu kutoka mwanzo. Wakati LAP ni mchakato unaoongozwa na serikali ya kitaifa, ni muhimu kuwa viongozi waliochaguliwa mashinani wanaelewa umuhimu wake. Kuunganisha masuala ya P/CVE na masuala mengine ya kupewa kipaumbele ambayo serikali ya mtaa inashughulikia inaweza kuwa mbinu nzuri, mradi tu miji inahakikisha kuwa haitii usalama katika masuala yasiyokuwa ya usalama. Kwa mfano, unaweza kueleza jinsi ambavyo ongezeko la visa vya utovu wa usalama unaathiri utalii, ama jinsi ambavyo vijana kutokuwa shuleni kunawatia katika hatari kubwa zaidi ya kusajiliwa katika VE.*

CAPs nyingi nchini Kenya hazifadhiliwi vya kutosha na kuzifanya kuwa wategemezi wa kupindukia wa wafadhili wa kigeni. Hali hii imeathiri uwezo wao wa uendelevu na kutenda kazi. Hali ingeweza kusuluhishwa kwa kiasi fulani kwa mawasiliano ya karibu na serikali za mitaa, ambazo zina uwezo wa kupata ufadhili wakati wa kuasisiwa.

***Funzo:*** *LAPs zinafaa kutungwa kwa njia ya kutumia kikamilifu rasilmali zilizoko bila kutegemea ufadhili zaidi. Washika dau walio na uwezo wa kupata rasilmali, za kimali na kifedha, lazima wahusishwe katika kutunga mchakato kwa njia ya maana.*

# Sura ya Tatu
## Kuanza na kutunga LAP

Huenda umehudhuria kipindi cha mafunzo cha SCN, ukasikia kuhusu ufanisi wa CAPs za Kenya, ama umeulizwa na serikali yako kutunga LAP. Bila kujali jinsi ulivyofika hapa, sasa unajaribu kuliwahi jukumu kubwa la kuandika LAP endelevu, yenye kuhusisha sekta nyingi, yenye kuwezekana na jumuishi. Sura hii inaainisha namna ya kubainisha msingi unaohitajika kisha kuandika LAP yako. Sura hii inajumuisha mifano mwafaka pamoja na viambatisho na nakala za kazi zilivyojazwa na vielelezo ili kukusaidia.

**Baada ya kusoma sura hii, hakikisha kuwa unaelewa:**

1. Umuhimu wa kupata uungwaji mkono wa wanasiasa.
2. Mchakato wa kukadiria hatari.
3. Namna ya kuweka kazi na majukumu ya jopo kazi la muda.
4. Hatua tano muhimu za kutunga LAP.

## 3.1 Bainisha Sababu ya kuwepo na LAP

### Pata uungwaji mkono wa kimkakati wa wanasiasa

Ili LAP ifanikiwe, inafaa kuwa jukumu la pamoja na wahusika katika serikali, ikiwa pamoja na viongozi wa mtaa, wabunge wa kitaifa na wafanya-maamuzi, hali kadhalika wahusika wasiokuwa wa kiserikali. Utekelezwaji wa LAPs unahitaji ushirikishi wa juhudi za sekta nyingi ili kuhakikisha ufanisi. Uuungwaji mkono wa kimkakati wa wanasiasa kuanzia mwanzoni ni muhimu ili kusheheni LAP katika miundo ya mitaa, sera na sharia. Kimsingi kuna vizuizi vitatu katika upatikanaji wa uungwaji mkono wa wanasiasa: (1) Kuelewa suala visivyo kutokana na kutojua; (2) kukosa ari ya kukabiliana na P/CVE kwa sababu masuala ya usalama ni jukumu la serikali ya kitaifa; (3) hofu ya kunyanyapaisha mji wako kwa kutekeleza waziwazi sera ya kuzuia itikadi kali au P/CVE.[9]

*Baadhi ya kaunti za Kenya zimesajili ufanisi katika upataji wa uungwaji mkono wa wanasiasa kwa kuelezea washikadau wa serikali kwamba huku ikiwa kwamba hawawajibikii usalama na amani katika kaunti, wanawajibikia vitu vinavyosababisha ukosefu wa amani na itikadi kali za ghasia. Kuzungumza na viongozi wa mtaa waliochaguliwa pamoja na tawi la serikali kuu kumekuwa muhimu sana katika kaunti zingine katika kufaulisha uungwaji mkono wa LAPs na wanasiasa kwa njia ya uendelevu.*

Upatikanaji wa uungwaji mkono wa wanasiasa unaweza kupatikana kupitia kwa njia tofauti tofauti, na barabara unayofuata itategemea miundo ya uongozi pamoja na mikakati iliyopo ya mtaa, ya kitaifa na ya kieneo. Matokeo yanafaa kuwa ya wajibu ulio wazi kutoka kwa viongozi wa kisiasa wa LAP pamoja na njia iliyokubaliwa na pande zote kwa mchango wa wanasiasa/kusahihisha wakati wa kuandika. Utetezi unaweza kuafikiwa kwa njia zifuatazo:

- ***Kimataifa:*** *Kumekuwa na msukumo wa kimataifa wa kutekeleza mitazamo ya kiasili ya usalama yenye mbinu laini za kuzuia. Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika na miungano mingine ya kimataifa inapigia debe mtazamo wa 'jamii-nzima' katika masuala ya amani na usalama. Washika dau wanaweza kutumia mtazamo huu wa kimataifa ili kushawishi serikali kukumbatia LAPs.*

- ***Kitaifa:*** *Iwapo serikali yako ya kitaifa imeanzisha Mpango wa Kitaifa wa P/CVE ama sera nyingine iliyo na jitihada za P/CVE, unaweza kutumia hii kama msingi wa kuzungumza na viongozi wa mtaa. Sio serikali zote za kitaifa zinatambua umuhimu wa serikali za mtaa katika mikakati yao. Hata hivyo, stakbadhi zao zinatoa msingi na vigezo vya LAPs – kwa mfano, ni kina nani ambao viongozi wa mtaa wanaweza kuzungumza nao na ni kina nani hawawezi kufanya hivyo nao.*

- ***Mtaa:*** *Serikali yako ya mtaa ina fursa ya kutumia uwezo wake wa kuitisha mikutano ili kupanga makongamano, au mikutano ili kutafuta msimamo wa pamoja miongoni mwa washikadau. Tukio hili hatimaye litainua uumgwaji mkono wa wanasiasa.*

- ***Mashirika ya kutetea haki mshinani:*** *Utetezi wa mashirika ya kimataifa yasiyokuwa ya kiserikali (INGOs), mashirika ya kutetea haki (CSOs) na wanaharakati pia wanaweza kusaidia kupata uungwaji mkono na wanasiasa kwa kudhihirisha ushahidi kuwa itikadi kali, ghasia na ugaidi unafaa kukabiliwa vyema zaidi kutoka mtaa wa nyumbani.*

- ***LAP Iliyojukumishwa:*** *Iwapo stakbadhi ya mkakati ya kitaifa inaainisha muundo wa mitazamo ya kimtaa, itakuwa rahisi kidogo kwako kuzungumza na serikali yako ya mtaa ili kuanza mchakato. Ukikumbana na changamoto, unaweza kutafuta serikali kuu ama wawakilishi wao ili watume maagizo kwa serikali yako ya mtaa iweze kushughulikia haja ya kutunga LAP.*

***Mfano: Human Rights Agenda (HURIA) na uundaji wa CAP ya Kwale.***

*Kaunti ya Kwale ilikuwa kaunti ya kwanza kuunda CAP – mchakato ulioanza hata kabla ya kuzinduliwa kwa NSCVE kirasmi. Mnamo mwaka wa 2016, HURIA, CSO ya nyumbani, ilitambua kuwa kaunti ya Kwale ilikuwa inashuhudia idadi kubwa ya vifo vinavyosababishwa na askari na watu kupotea kwa lazima, mambo yaliyohusishwa na tuhuma za itikadi kali za ghasia au makundi yanayounga mkono itikadi hizo. Jambo hili lilikuwa linasababisha mgogoro na mvutano katika jamii. HURIA iliamua kufanya mikutano na wanavijiji ili kuelewa masuala nyeti yaliyokuwa yakikumba jamii kwa nia ya kujua namna ya kuyakabili. HURIA ilizungumza na serikali ya mtaa na serikali kuu ili kuunga mkono uundaji wa mpango wa kukabili masuala haya. HURIA ilitumia mbinu ya utetezi kwa uzito sana miongoni mwa wenyeji na kwa serikali ili kupata uungwaji mkono katika uundaji wa CAP ya kwanza.*

## Andaa makadirio ya hatari ya mtaa

Ukishapata uungwaji mkono wa wanasiasa katika kiwango cha mtaa na cha kitaifa, mji wako utahitajika kung'amua iwapo LAP inahitajika au la. Serikali ya mtaa inahitajika kuanzisha makadirio ya hatari ya mazingira ya vitisho. Kikundi kilichoteuliwa kukamilisha mkadirio ya hatari sharti kijumuishe ama kuzungumza na wawakilishi kutoka sekta zote zilizo na uhusiano na P/CVE, pamoja na jamii ambayo LAP inanuia kuhudumia.

Kuna mbinu nyingi za kukadiria hatari za mtaa. Undani wa tathmini yako ya hatari ya mtaa itategemea rasilmali za kifedha zilizoko na kiwango cha vitisho kilichotarajiwa awali. Makadirio ya hatari ya mtaa sharti yawe na usawasishaji: lazima ifanye kazi kwa undani lakini isichoshe washikadau au kutumia rasilmali zote. Uangalizi wa ndani wa hali utafanyika kama kiwango cha vitisho kinafikiriwa kuwa cha juu kiasi cha kutaka kuanzisha LAP.

Inapendekezwa kuwa tathmini iangazie yafuatayo:

- *Tambua **hali** na **kiwango** cha hatari za itikadi kali za ghasia mtaani.*
- *Elezea **namna ambavyo** waendeshaji wa mtaani wa itikadi kali za ghasia wanaojulikana wanavyoweza kuongeza viwango vya hatari.*
- *Tenga sababu za hatari za mtaani kulingana na zile **zinazotokana na, na kutoka kwa:** watu binafsi, itikadi na taasisi.*

Unapoangazia watu binafsi, tathmini inafaa kuzingatia watu walio kwenye hatari zaidi na makundi yanayodhaniwa kuwa hatari kwa jamii. Tathmini hii ya hatari ya mtaa inafaa kusaidiwa na utafiti uliofanywa ama ule mpya na uchanganuzi wa sababu za mtaani za kusukuma na kuvuta zinazowafanya watu kuingia katika misimamo mikali ya ghasia. Itikadi husaidia kutambua na kuelewa kimuktadha mazingira ambamo makundi ya misimamo mikali ya ghasia yanafanyia kazi. Kwa taasisi, zilizo rasmi na zisizo rasmi, zinafanya kazi kama dira ya kuonyesha mitandao iliyoko na ni muhimu ili kuonyesha makundi ya misimamo mikali ya ghasia na makundi yaliyo katika hatari ya kushambuliwa yalipo.

## Anzisha jopo kazi la muda

Kama makadirio ya hatari ya mtaa yanaonyesha kiwango cha juu cha vitisho na kubaini kuwa LAP inahitajika, hatua inayofuata ni kuanzisha jopo kazi la muda ili kuongoza uundaji wa LAP. Serikali ya mtaa inafaa kutambua na kufikia washikadau wote wanaofaa ili kuunda jopo kazi la muda. Jopo kazi la muda linahitajika kuwa na usawa wa kijinsia na kujumuisha vijana na wanawake katika nafasi za uongozi. Uanachama unaweza kutoka katika taasisi za serikali za mtaa na serikali kuu, mashirika ya kijamii na mashirika ya mashinani, mashirika ya kimaeneo na ya kimataifa, viongozi wa kijamii, viongozi wa makanisa, vijana wenye ushawishi, watafiti, vyombo vya habari, mashirika ya kibinafsi na wataalamu wa mtaa wa maendeleo ya mtaa au maisha. Ni muhimu kuhusisha washikadau na washawishi wanaoweza kutambua na kufanya kazi na vijana ambao hawaenzi vianzo asilia vya utawala.[10]

Jopo kazi la muda linafaa kuanzishwa kwa amri rasmi, ama yenye nafasi sawa, ili kuhakikisha uhalali na mchakato wazi. Amri ni sharti iwe na sehemu zifuatazo:

- *Orodha ya taasisi, mashirika na wataalamu wanaoshiriki katika jopo kazi la muda.*
- *Taarifa za watu kutoka katika hizo taasisi, kukiwa na maelezo faafu ya vyeo vyao na stadi zinazofaa P/CVE.*
- *Jina la mwenyekiti wa jopo kazi la muda, ambaye atashirikisha kazi – ikiwezekana afisa kutoka kwa afisi ya meya au gavana, ama idara katika serikali ya mtaa anayehusika na masuala ya P/CVE.*
- *Sheria na maagizo, ama 'masharti ya kazi,' kwa kazi ya kikundi kazi cha muda – ikiwa pamoja na itifaki za mikutano, kubadilisha wanachana na ufanyaji wa maamuzi.*
- *Wajibu ikiwa pamoja na rasilmali zilizokubaliwa ili kuandika mpango na kazi na majukumu.*
- *Makataa ya kumaliza shughuli kutokana na wajibu wa jopo kazi la muda.*

***Mfano: Kikundi kazi cha jamii ya Kumanovo***

*SCN ilisaidia manispaa ya Kumanovo kuanzisha shirika la sekta nyingi la kushirikisha – CAT – kuandika na kutekeleza sera na mpangilio wa P/CVE. Kwa kufanya kazi na taasisi zilizopo, CAT ilianzishwa kirasmi kwa amri ndani ya Baraza la Mtaa la Kuzuia, kitengo kinachofanya kazi zinazohusu masuala yote ya uzuiaji katika manispaa, kama jopo kazi la kudumu lenye wajibu wa kuandika na kutekeleza kazi mpango ya mtaa ya P/CVE. Amri iliyoanzisha CAT inataja waziwazi taasisi ambazo zimejumuishwa katika kazi yake na zinatarajiwa kutuma mwakilishi. Jambo hili linahakikisha kuwa washikadau wote faafu na utaalamu wao wamejumuishwa wakati wa kuandika sera ya mtaa kwa njia ya mashiko zaidi. Pindi stakbadhi ya sera ilipoandikwa, wanachama wa CAT waliiwasilisha katika Baraza la Mtaa la Kuzuia, ambapo ilikubalika kwa amri. Yote haya yanahakikisha kuwa kazi hii inakubalika katika mifumo na taasisi, jambo ambalo linasaidia kukumbatia, uwajibikaji na uendelevu wa kazi inayohitajika kutekelezwa kutokana na LAP.*

# 3.2 Tunga LAP

## Hatua ya 1: Fanya uchanganuzi wa hali

LAPs zinafaa kujengeka kwenye msingi wa utafiti na kutumia mtazamo wa ushahidi ili ziweze kulenga ndipo na kuleta matokeo ya kupimika. Jopo kazi la muda sharti liongoze katika uchanganuzi wa hali, ambayo sharti ishughulikie yafuatayo:

- *Tambua vitisho vya nyumbani, mambo yanayosukuma na watu walio hatarini, kujenga kwenye tathmini ya hatari za nyumbani.*
- *Sahihisha sera, miundo na shughuli ambazo zinatekelezwa wakati huo ambazo zinahusiana na P/CVE.*
- *Angazia rasilmali za kifedha na za kibinadamu zilizopo na ambazo zina majukumu ya kushughulikia P/CVE na masuala yote faafu yanayotagusana na misimamo mikali, chuki na ugaidi.*
- *Angazia shughuli za mashirika ya kijamii zinazosaidia kazi za serikali.*
- *Elewa mapengo ya kitaalamu na uzuri wa wahusika wanaofanya kazi katika uwanja huu.*
- *Tambua na kuchanganua maelezo ya watu wenye misimamo mikali ya mtandaoni na yasiyo ya mtandaoni (hii huenda ikawa sehemu mahsusi ya msingi wa ushahidi ambapo rasilmali na hitaji vinahitaji uchanganuzi wa kindani wa kidijitali.*
- *Tambua walengwa wa kunufaika kutokana na LAP yako.*
- *Tambua sababu zozote za kisiasa au za kijamii ambazo huenda zikaathiri ufanisi wa mradi wako, ama kichanya au kihasi; kwa mfano, mabadiliko katika usalama au sera faafu za serikali.*
- *Chunguza mitazamo ya umma kuhusu misimamo mikali kupindukia na kipimo cha ustahimilivu, ikiwezekana katika makundi ya kidemografia na ujirani na kutumia sampuli zisizokuwa na upendeleo.*
- *Weka matokeo ya uchunguzi katika muktadha wa uchanganuzi ndani ya mizani ya kihistoria, kisiasa, kijamii na kiuchumi.*

Jopo kazi la muda sharti kwanza lipange kuwa na mjadala ili kutambua washikadau wakuu katika jamii za mtaani. Hili jopo kazi linaweza kutumia mbinu ili kuelewa mahitaji tofauti tofauti ya jamii. Kwa mfano, mawasilisho kutoka taasisi kuu, makundi lengwa, mahojiano makuu ya kupata siri, uchunguzi wa nyumba hadi nyumba, uchunguzi wazi wa majukwaa ya kidijitali ya washikadau, uchanganuzi wa matawi wa changamoto, mapitio ya maandiko yaliyoko, na uzuri, unyonge, fursa na vitisho (SWOT).[11]

> *Tumia wasomi na wataalamu wa nyumbani unapofanya uchanganuzi wa hali. Msaada wa kitaaluma kutoka nje unafaa kutumika tu kujaza mianya maalum na kufundisha washikadau wa kiasili ili kufanya mchakato kuwa endelevu kinyumbani hali inapoendelea. Kizazi cha kwanza na cha pili kilitilia mkazo sana utaalamu wa kinyumbani, unaoendeleza uelewaji wa kinyumbani na ukubalifu. Kizazi cha tatu cha CAPs, ama RCAPs, kilitegemea wataalamu wa kiwango cha kitaifa walioongoza katika RCAPs nyingi, ambazo katika hali zingine zilipelekea kuwepo kwa stakbadhi za sampuli za kupachika ambazo hazikuwakilisha kwa kindani masuala ya mtaa na maitikio.*

Yaliyomo —

## Hatua ya 2: Andaa Nadharia ya Mabadiliko (ToC)

Ni muhimu kwamba LAP inayoongozwa na ToC isheheni lengo lililo wazi na matokeo yanayotarajiwa kuafikiwa ndani ya muda mfupi na muda wenye urefu wa kadri. Muundo thabiti wa ufuatiliaji na tathmini unahitajika ili kupima ufanisi na kuhakikisha kwamba shughuli za LAP zinafanya kazi ili kulingana na lengo na matokeo. Sura ya tano ya ala hii ya zana inashughulikia ufuatiliaji na tathmini kwa undani zaidi; kielelezo cha kuandaa ToC kinapatikana katika Kiambatisho F, na jedwali la kuonyesha ufuatiliaji linapatikana katika Kiambatisho G.

Mkakati mzuri unafaa kujengwa kwenye msingi wa ushahidi. Hata hivyo, ukosefu wa wakati wa kutosha wa kupanga ama bajeti na ukosefu wa ufahamu wa kiufundi mara nyingi humaanisha kuwa ufuatiliaji na tathmini unachukuliwa kama mzigo na kupuuzwa hadi awamu ya kufunga mradi. Wakati mwingine ufuatiliaji na tathmini vinapuuzwa kabisa. Katika visa vingine, vinaweza kuchukuliwa kama kazi ya kisanduku cha kuweka alama tu, na mara nyingi kupewa wataalamu wa ufuatiliaji na tathmini.

Ili kuhakikisha athari ya kupimika kwa walengwa na kusheheni LAP na msingi thabiti wa ushahidi, ni muhimu kwamba upimaji na tathmini isichukuliwe kama jambo la kuchagua kufanya bali lishindiliwe katika miradi kutoka mwanzo. Kuingiza ufuatiliaji na tathmini katika mchakato wa muundo wa LAP una manufaa kadhaa:

- *Kuna kuruhusu kupima ufanisi dhidi ya malengo na kubaini iwapo mwingilio wako unafanya kazi kama ilivyotarajiwa, au kama kuna mabadiliko yanayofaa kufanywa.*
- *Kutakusaidia kuelewa iwapo athari ya LAP yako kwa walengwa na jamii pana wanamoishi, na kama LAP yako inaleta matokeo yasiyotarajiwa.*
- *Kunatoa mafunzo yaliyopatikana, kukuruhusu kufanya marekebisho kwenye LAP yako ili kukabiliana na changamoto.*
- *Kunaongeza uwezo wako wa kujifundisha kutoka kwa shughuli na kuhakikisha kuwa athari kubwa inapatikana katika kila kazi mpya.*
- *Kunatangaza kusudi la wazi na thamani ya LAP yako, itakayokusaidia kupata ufadhili, kupata washirika na kuongeza uwezo wako wa kufikia jamii.*

Kutengeneza ToC ni hatua muhimu zaidi katika uundaji wa mpango wa LAP wa ufuatiliaji na tathmini. Utengenezaji wa ToC faafu kutakukupatia kitu cha kukusudia na kukusaidia kueleza maana ya ufanisi katika LAP yako. Bila LAP iliyo wazi, inaweza kuwa vigumu kuelewa kile ambacho LAP yako imefanikiwa kupata na iwapo imeleta tofauti ya kupimika katika walengwa.

LAP inahitajika kukubaliana na sera na mikakati ya serikali ya kitaifa na serikali ya mtaa na kuhakikisha kuwa inafuata mbinu zana zilizopo, kama kuna yoyote inayofaa. Aidha, ili kuhakikisha uendelevu na msaada kutoka taasisi za kitaifa, jopo kazi la muda linahitaji kutafuta uunganikaji wa shughuli na bajeti pamoja na mipangilio ya maendeleo. LAP haina haja ya kuwa stakbadhi ya kusimama peke yake na yahitaji kujumuishwa katika vianzo vya ufadhili pale panapowezekana.

***Mfano: Jitihada za Kiunga Youth Bunge Initiative (KYBI) na Kikozi Programme Group ili kufanya ufuatiliaji na tathmini kikamilifu kwa hadhira isiyoweza kusoma wala kuandika.***

*Katika juhudi za kuandaa majukwaa kwa vijana ili kuzungumza na CAP ya Lamu, KYBI na Kikozi, mashirika mawili ya misingi ya kijamii (CBOs) kutoka katika kaunti ya Lamu, Kenya, yaliunda majopo kazi ya vijana ya P/CVE katika kiwango cha wadi. Katika mkutano wao wa kwanza na vijana, walikabiliana na changamoto ya kupambanua ufanisi wa hafla, kwa vile walikuwa na ugumu wa kujibu maswali ya uchunguzi wa kabla na baada ya hafla. Wengi wa vijana hawakuwa na uwezo wa kusoma na kuandika, na wengi walikuwa na shida ya kuelewa maswali, ambayo yalitungwa kwa kutumia istilahi za ufuatiliaji na tathmini. KYBI na Kikozi waliamua kwamba, kwenda mbele, wangefuata mbinu zisizozoeleka za uchunguzi wa kabla na baada ya hafla. Timu inayoongoza muradi ilianza kutunga upya maswali ili yawe rahisi kuelewa na pia wakawa na mijdala ya makundi na washiriki ili waweze kupima ufanisi wa hafla zao.*

## Hatua ya tatu: Fanya ushauri na jamii

Kwa kuwa jamii ya kiasili ndilo kundi la kunufaika na LAP, jopo kazi la muda linafaa kuandaa mashauriano na jamii ili kuhakikisha kuwa umma unachangia na kuikumbatia. Jambo hili ni muhimu katika kutekeleza mtazamo jumuishi wa 'mji-mzima.' Mashauriano haya yanafaa kuwa mseto wa makongamano makubwa ya maendeleo na mikutano midogo midogo. Vitu muhimu vya kuzingatia:

- *Kuwa na vipindi vya mafunzo kuhusu madhihirisho ya P/CVE na VE ili jamii ielewe masuala na umuhimu na thamani ya kuwa na LAP.*
- *Kufanya washikadau wakuu kueleza mji wanaotaka na kuelezea maono yao ya siku za usoni.*
- *Kuidhinisha tathmini ya hali ili kupata uelewa wa ndani.*
- *Kuidhinisha ToC.*
- *Kukusanya maoni kuhusu suluhu zinazotoka kwa mtaa na majibu yaliyoko mashinani kuhusu masuala ya P/CVE.*

Mtazamo maalum unafaa kutolewa kuhakikisha kuwa washika dau kutoka sekta zilizo-ngumu-kufikiwa zinahusishwa. Ngumu-kufikiwa inaweza kutambuliwa kwa misingi ya eneo la kijiografia, kama vile eneo la mashambani, ama makundi yaliyotengwa, yaani makundi ambayo kwa kawaida hayajumuishwi katika masuala ya umma ama ambayo kwa kawaida wanatuhumu serikali. Mikutano midogo ikifanyika katika maeneo ya jamii hizi inaweza kufikiwa na makundi ya ngumu-kufikiwa.

*Uteuzi wa washikadau unafaa kufanywa na kundi zima la jopo kazi la muda wala sio na mwenyekiti au mshikadau mmoja. Kaunti zingine za Kenya, wakati wa kutengeneza CAPs zao, yalifanya kamishna wa kaunti kuongoza uteuzi wa washikadau ili kufanya ushauri, hususan wakati wa kutengeneza RCAPs. Jambo hili lilileta uhasama katika jamii, kwani kamishna alionekana kuwa na mapendeleo badala ya kusikiliza moja kwa moja kutoka kwa wanachama wa jamii ambao stakbadhi inanuia kuhudumia.*

Yaliyomo —

***Mfano: Pastoralist Women for Livelihood and Social Support (PWLS) na mazungumzo na jamii zilizo 'ngumu-kufikia.'***

*Shirika lenye misingi ya kijamii CBO) kule Isiolo, liligundua kuwa wanawake wafugaji walikuwa wakiachwa nje ya kampeni za uhamasishaji kuhusu CVE ama jitihada za kuzungumza na jamii juu ya masuala ya CVE. Wanawake wafugaji kule Isiolo wameathirika sana na itikadi kali za ghasia na wengi wana ndugu wa familia wanaoshutumiwa kwa kusaidia al-Shabaab, ama kutoka Isiolo ili kujiunga na kikundi. PWLS iliandaa misururu ya mikutano na wanawake ili kuangazia mwanya huu. Ili kuzungumza na kundi hili 'ngumu-kufikia,' waliandaa mikutano katika sehemu zilizokuwa zikitembelewa zaidi na wanawake. Walitumia istilahi za mtaani kuelezea jitihada za CVE, wakapata uhusika wa chifu wa mtaa, na kuajiri washirikishi ambao wanawake wangekuwa huru kuzungumza nao.*

## Hatua ya nne: Anzisha miundo ya ushirikishi – muunganiko wa mtaani wa kuzuia (LPN)

Kuna mifumo na miundo mingi ambayo inaweza kutumika kama misingi ya kupima ufanisi wa ushirikishi na utekelezaji. Kwa kijumla, miundo ya ushirikishi sharti iitikie ipasavyo kipimo cha vitisho, kupima rasilmali zilizoko na mahitaji na kuhakikisha upatanisho wa taasisi na majukwaa yaliyoko. Panahitajika kuwa na masharti ya kazi (ToR) wazi ama stakbadhi ya njia za wastani za kufanya kazi (SOPs) kwa miundo yote ya ushirikishi ambayo inafafanua majukumu na wajibu wa nafasi za uongozi na taasisi. Stakbadhi hizi sharti zihusishe kiwazi mbinu za uwajibikaji. Maelezo kama vile sheria za maadili, itifaki za kupasha habari, idadi ya mikutano na ifanyike lini na namna ya kutoa ripoti ni lazima iafikiwe. Picha ya muundo wa ushirikishi wa Kenya unaweza kupatikana katika ukurasa wa 12.

Bila kujali ukubwa na uchangamano, miundo ya ushirikishi sharti ijumuishe kamati za sekta nyingi inayohusisha wafuatao. SCN inatumia istilahi LPN kuelezea hii kamati.

- *Mwenyekiti ama wenyekiti wenza wa kamati.*
- *Mwakilishi kutoka kwa serikali ya mtaa*
- *Mwakilishi kutoka kwa serikali kuu.*
- *Sehemu pana ya washikadau wanaofaa, kama ilivyopendekezwa kwa jopo kazi la muda katika sehemu ya 3.1. Watu mahsusi, taasisi na mashirika yanaweza kubadilisha ama kuongeza idadi.*

*CEFs katika kaunti nyingi za Kenya zilipata ugumu katika kusonga mbele na utekelezaji wa CAP kwa sababu wawakilishi wa serikali waliochaguliwa kuketi katika kamati wakati mwingine hawakuwa wakipatikana kuhudhuria mikutano ama hawakuwa wakihudhuria mara kwa mara na kwa hivyo kutoweza kushughulikia vipengele muhimu vya mikutano. Uhamisho wa mara kwa mara au kupewa majukumu mengine kwa maafisa wa serikali kuliharibu hali hata zaidi. Ni muhimu sana kwamba wawakilishi wa serikali wanaoteuliwa kukaa katika vikao vya LPN kusawazisha kati ya kuwa na nyadhifa kuu sana kuweza kufanya maamuzi na kupata wakati wa kutosha ili kutimiza majukumu yao kama ilivyoelezwa katika ToR. Huku maafisa wa ngazi za chini wakiweza kuwa na wakati mwingi zaidi, wao kutoweza kuathiri waamuzi wa ngazi za juu ama kufanya maamuzi kwa mitazamo yao huathiri uwezo wa kamati kutekeleza LAP.*

*Maafisa wa ngazi za juu wana mamlaka ya kuidhinisha maamuzi na shughuli; hata hivyo, mara nyingi huenda wasipatikane kwa kazi za kamati, kwani wanasimamia vitengo vingi.*

**Je, ninahitaji kuwa na mshirikishi wa mtaani wa kuzuia?**

*Iwapo rasilmali zinapatikana na vitisho vya VE viko juu, sharti serikali ya mtaa iajiri mshirikishi wa P/CVE ili atumike kila siku. Kama rasilmali hazipo, mameneja wakuu lazima waunganishe kazi za LPN kwa kazi za mwakilishi ili kuhakikisha kuwa wanatenga muda ili kuangazia utekelezaji wa LPN na LAP.*

Iwapo LPN ina zaidi ya wanachama 20, sharti ufikirie kuunda kikundi kidogo ili kusaidia katika ushirikishi. Kamati hiyo ndogo lazima iwe na mwenyekiti ama wenyekiti wenza, wawakilishi wa serikali ya mtaa na serikali kuu na kuchagua washikadau kutoka katika kundi pana la washikadau. LPN yenye wanachama wa kudumu wasiozidi 12 wamedhihirisha kuwa idadi mwafaka katika baadhi ya sehemu ambazo SCN imejaribia suala hili.

Kwa miji yenye idadi kubwa ya watu ama viwango vya juu vya vitisho, huenda ukataka kupanga LPN katika kamati ndogo ndogo ili kusaidia ushirikishi na utekelelezaji wa LAP. Kamati ndogo ndogo zinaweza kuundwa kwa misingi ya sehemu ya kijiografia kama vile maeneo madogo ya mji, ama eneo la mafunzo.

*Kaunti nyingi za Kenya zimeweza kuwa na utekelezaji kwa kuunda wasimamizi mihimili. Nchini Kenya, shughuli za CAP zimepangwa katika mihimili ya maudhui kama vile: elimu, utamaduni ama uchumi. Wasimamizi mihimili wanawajibika na kushirikisha shughuli na kufuatilia maendeleo katika sehemu zao mahsusi za kazi. Jambo hili linasaidia sio tu ushirikishi wa shughuli lakini pia uwezo wa washikadau kuchanganua ufanisi wa CAP.*

**Mfano: Kuanzisha LPNs nchini Jordan na Lebanon**

*Ikiwa imechochewa na kielelezo cha Denmark cha 'Schools-Social Work-Police (SSP)', manispaa sita kutoka kote nchini Jordan na Lebanon walianzisha kirasmi SCN ya kwanza mnamo mwaka wa 2017, wakitumia miundo iliyoundwa kwa ajili ya kushughulikia kisa cha sekta nyingi ili kuzuia katika kiwango kisichokuwa cha msingi. Mkutano uliitwa mwanzoni na mameya, LPNs zilisajili wanachama kutoka makundi ya mtaani ya kidini, elimu, vijana, maendeleo, afya na maslahi. Majukumu mahsusi na usuli vilikuwa tofauti kutoka manispaa moja hadi nyingine, na LPNs zote zilihitajika kudhihirisha sura tofauti za manispaa kijamii, kikabila na kidini pamoja na kijinsia. Kisha wanachama wa LPN walichagua kiongozi wa kuongoza ushirikishaji na manispaa, kuwakilisha LPN katika taasisi zingine, kuitisha mikutano na kuidhinisha mkakati na stakbadhi za mpango kazi.*

***Mfano: Kuanzisha LPNs nchini Jordan na Lebanon***

*Viongozi wa LPN wanaendelea kuwa muhimu katika ufanisi wa miundo, kukuza uongozi na stadi zao za kazi kumesaidia kupanua kuaminika na kukumbatia taasisi na kuanzisha taratibu za kufunza-mfunzaji kupitia kwa uongozi na wanachama wengine wa LPN wanafundisha wenzao katika manispaa nzima. LPNs katika nchi za Jordan na Lebanon zimechochea kuanzishwa kwa zingine kwingine ulimwenguni, kupitia kwa mipangilio ya LPN na kupitia kuchochea miji mingine wanachama utekeleza mipango kama hii. Kwa sasa wanawakilisha miundo ya kimsingi ya kufahamisha na kufaulisha mikakati ya kitaifa ya P/CVE katika kiwango cha mtaa katika nchi zote mbili na sasa wanajenga miundo yenye utofauti ya ufundishaji-wenza wakiwa na miundo ya 'Nyumba Salama' kote nchini Netherlands.*

## Hatua ya tano: Halalisha na kutunga sheria

Sharti LAP yako iwe na usawazisho kati ya kuwa fafanuzi na kuweza kugonga ndipo ili iweze kufikiwa na jamii ambayo inanuia kuhudumia. Kiwiliwili cha LAP kinaweza kupatikana katika Kiambatisho D. Baada ya kutunga LAP, itahitajika kuhalalishwa na washikadau wahusika. Jambo hili linaweza kufanywa kwa njia ya mtandao kwa kurejelea na kuweka pamoja maoni, kupitia kwa warsha, ama kupitia kwa misururu ya mikutano – ama kupitia kwa mchanganyiko wa mbinu zote tatu. Washikadau wa kuhusishwa lazima wawe pamoja na:

- *Viongozi wakuu wa serikali za mtaa pamoja na/ ama viongozi waliochaguliwa.*
- *Wawakilishi wa serikali kuu kama vile maafisa wa ugatuzi na maafisa wa usalama wanaohudumu katika mji au eneo.*
- *Jopo kazi la muda.*
- *Wanachama wateule wa jamii kutoka kwa wale walioshiriki katika mazungumzo.*

Ili kuifanya LAP kuwa rasmi, ya kutekelezeka na endelevu, ni jambo la umuhimu mkubwa kuweka stakbadhi katika sheria na miundo ya kisera. Viongozi wa kisiasa waliochaguliwa wanaofanya kazi kwa kutetea maslahi ya wapiga kura wao wanaongeza uhalali ulio muhimu kwa stakbadhi kwa kuhahakikisha kuwa LAP inapata nguvu kutoka wa miundo ya kitaasisi na ya kisheria iliyoko. Hii ni muhimu ili kujenga ukubalifu wa kinyumbani na kuweza kufanya kazi kwa muda mrefu.

*Kaunti nyingi za Kenya ziko katika harakati za kuptisha miswada ya 'amani na mshikamano' katika mabunge ya kaunti zao. Miswada hii inashughulikia vitu vingi lakini pia inarejelea CAPs ama michakato ya P/CVE. Kupitia kwa mswada huu, washikadau wameweza kuzungumza na viongozi waliochaguliwa kuhusu umuhimu wa michakato inayoongozwa kutoka nyumbani na kuelezea upya masuala ya P/CVE ili viongongozi waliochaguliwa wavutiwe na kuona umuhimu wake katika kunufaisha wapigaji kura wao. Miswada hii pia itawezesha kutilia maanani CAPs kwa wakuu wa kaunti kuleta uwezekano wa ufadhili wa CAPs kutoka kwa kaunti.*

Kulingana na mfumo wa uongozi na miundo husika ya taasisi na sheria, njia mahsusi ya kuingiza LAP itakuwa tofauti. Sheria ya LAP haihitaji kuwa ya kusimama kipweke. Kwa mfano, inaweza kujumuishwa katika mabadiliko ya sera, kipengele cha ziada ama ala ya ziada chini ya sera zingine husika zinazohusu ghasia za miji, ushikamano ama amani na usalama. Baadhi ya mifano ni pamoja na:

- *Tamko kuu ama amri kutoka kwa meya au gavana.*
- *Sheria ama mswada uliopitishwa na bunge.*
- *Sera inayoungwa mkono na mkuu wa idara ya mji kama vile waziri, katibu ama afisa mkuu.*
- *Sahihi ya kuunga mkono kutoka kwa mwakilishi wa serikali kuu, kama vile waziri wa ugatuzi ama huduma za usalama.*
- *Hati za makubaliano baina ya idara za serikali.*
- *Taarifa ya kuidhinisha kutoka kwa meya, gavana ama kiongozi mwingine aliyechaguliwa.*
- *Amri zingine zilizotolewa chini ya sheria kuu ama sheria ndogo.*

*Kaunti zingine za Kenya kama vile Mombasa na Mandera zimeanzisha afisi za P/CVE kwa amri kuu ya gavana. Jambo lili limehakikisha kuwa kuna afisa mkuu anayewajibikia masuala ya P/CVE. Kama ilivyotajwa hapo juu, kama rasilmali zinaruhusu na viwango vya vitisho viko juu, kuteua mshirikishi kiongozi wa kuzuia linaweza kuwa jambo muhimu katika utekelezaji wa LAP.*

***Mfano: Midrift Hurinet na uundaji ya Sera ya Kuzuia Ghasia katika Kaunti ya Nakuru***

*Katika wakati wa kutekeleza Mpango wa Sekta Nyingi wa Kuzuia Ghasia katika Sehemu ya Mji (IUVP) unaoongozwa na Midrift Hurinet, iligundulika kuwa kulikuwa na masuala mengi yaliyofichika ambayo huenda yasiweze kushughulikiwa katika uhai wa mradi na ambayo yalihitaji mtazamo wa sekta nyingi na kuwa na muundo wa sera. Masuala ibuka yalikuwa na muunganiko, na yalihitaji mpango mpana wa kuzuia ghasia. Washikadau walitafutwa wakati wa mijadala ya kila wadi ili kutambua masuala ambayo sera ya kuzuia ghasia ingeshughulikia. Masuala yalijadiliwa zaidi na mikutano ya manispaa ili kupata uhalalishaji kutoka kwa washikadau waliotoka katika kikosi cha polisi, mashirika ya kutetea haki na viongozi wa vijana. Katika warsha za baadaye za uhalalishaji, PCVE ilitambuliwa kama suala ibuka na kwamba inafaa kujumuishwa katika sera. Sera ya Kuzuia Ghasia ya Kaunti ya Nakuru ilichangia uundaji wa CAP na inaendelea kuchangia mikutano ya utekelezaji wa CAP. Hasa, inachangia katika utafutaji wa rasilmali, pale ambapo Mswada wa Amani ambao uko mbele ya bunge la kaunti, unapania kufanya rasmi uzuiaji wa ghasia katika Seikali ya Kaunti ya Nakuru.*

# Sura ya nne

## Kutekeleza LAP

Kutunga LAP na kuanzisha miundo ya kushirikisha na kutekeleza huenda kukadhaniwa kuwa rahisi ukilinganisha na kutekeleza kwenyewe. Serikali zinaweza kuwa nzuri sana katika uandishi wa stakbadhi, lakini utekelezwaji aghalabu huwa jambo changamano na lenye shida.

Sura inayofuata inakuongoza kupitia kwa mchakato wa kuzindua LAP, kupasha habari kwa washikadau kuhusu yaliyomo, kutengeneza kazi mpango ya kila mwaka na kutoa msaada wa sera inayofaa. Pia tutaangazia uwezekano wa njia nne za ufadhili wa kifedha wa LAP yako – rasilmali zilizoko, bajeti za serikali, fedha kutoka kwa wafadhili na ushirikiano na mashirika ya kibinafsi. Kumbuka kuwa LAPs zote sharti ziafikike ndani ya ufinyu wa rasilmali zilizoko na kuangazia hitaji ipasavyo. Sehemu ya mwisho ya sura hii inaangazia umuhimu wa kukadiria athari ya LAP kila mwaka, kuunda kazi mpango ya kila mwaka, kuingalia upya miundo shirikishi na kuwa na toleo jipya la tathmini ya hatari na LAP kama inavyohitajika.

**Baada ya kusoma sura hii, hakikisha kuwa unaelewa:**

1. Jinsi ya kuzindua LAP yako na kuwasilisha ujumbe kwa jamii kuhusu yaliyomo.
2. Jinsi ya kutengeneza kazi mipango za kila mwaka zinazowezekana na zenye kupimika.
3. Njia nne za kufadhili LAP yako kifedha.
4. Jinsi ya kukadiria athari ya LAP.

## 4.1 Kuzindua na kuwasilisha ujumbe wa LAP

### Andaa hafla ya kuzindua

Ni muhimu sana kwa ufanisi wa LAP kuitangaza katika jamii. Ufahamu wa mbinu za nyumbani za kuzuia na mwitiko wa taasisi zimedhihirishwa kuwa sehemu muhimu za njia za kijamii za ustahimilivu.[12] Kwa kwaida, shirika lile lililoipa LAP nguvu za kisheria pia litakuwa mwenyeji wa hafla ya uzinduzi. Ni muhimu kuwa na wawakilishi wa washikadau wote kushiriki katika mchakato wote, pamoja na vyombo vya habari, viongozi wa kisiasa wa mtaa waliochaguliwa na jamii pana kuwa katika sherehe ya uzinduzi. Hii ni fursa ya kwanza kuwasilisha LAP iliyokamilishwa kwa jamii, kwa hiyo ni muhimu kuonyesha kuwa mchakato umekuwa jumuishi kufuatana na mtazamo wa 'mji-mzima.' Uwe tayari kujibu maswali na kufafanua. P/CVE ni mada tete, kwa hiyo ni muhimu kuonyesha kuwa hiyo sera inahimiza umoja wa kijamii na sio kuleta unyanyapaa ama kuangazia tu sehemu ndogo ya jamii.

## Toa taarifa kuhusu LAP

Hata kama mji wako ni mdogo, haiwezi kuchukuliwa kuwa sherehe ya uzinduzi pekee inatosha kuhamasisha jamii yote na walengwa wote kuhusu LAP. Jopo kazi litahitajika kuandaa msururu wa shughuli za kutoa taarifa ili kuhakikisha kuwa umma na washikadau tofauti tofauti wanapata ufahamu kuhusu LAP na athari na maendeleo yake. Mawasiliano yanafaa kujumuisha yafuatayo:

- *Busara ya kuwa na LAP.*
- *Yaliyomo katika LAP na hatua za utekelezaji.*
- *Hatua za uwajibikaji, ikiwa pamoja na kazi za washikadau tofauti tofauti.*
- *Mafunzo na uhamasishaji wa P/CVE.*
- *Habari kuhusu maendeleo yaliyofanywa na mabadiliko yoyote katika LAP.*

*Zingatia habari za kidemografia za mji wako wakati wa kutunga mpango wa mawasiliano. Kwa mfano, Serikali ya Somalia ilitumia mtindo-wa-vichekesho katika machapisho ili kuelimisha umma kuhusu kazi mpango yao ya kitaifa kuhakikisha kuwa watu wasiojua kusoma na kuandika wanaweza kupata ujumbe wa makakati.*

Kampeni za mawasiliano pia zinasaidia kuongeza imani miongoni mwa watoa huduma, mashirika ya kijamii, serikali na jamii. Kujenga-imani ni kazi inayoendelea; mawasiliano ya mara kwa mara yaliyo jumuishi yanafaa kuendelea katika hatua zote za utekelezaji. Vizuizi vingine vya utafutaji wa washirika haviwezi kuepukika. Hivi vinaweza kuwa pamoja na vizuizi vya kitaasisi ama washirika wengine kutokuwa na ari ya kuzungumza au kutoa taarifa. Ni muhimu kusema kwamba washikadau wengi waliotafutwa katika LAP watakuwa tayari wako na mipango mingine ya kazi, kwa hiyo jopo kazi sharti litilie mkazo kusudi la LAP kuingiana, kujenga juu ya na kuongezea nguvu ujuzi wao na kazi zinazoendelea.[13]

*Makadirio ya hali na mchakato wa uandishi wa CAPs za kizazi cha pili nchini Kenya ilikuwa jumuishi na ya kina sana. Washika dau wengi na wanachama wa jamii walihusishwa. Mara ya kwanza, stakbadhi zilichunguzwa sana, lakini baadaye kidogo wakahusisha mitazamo isiyokuwa ya usalama kufuatia mazungumzo na mashirika ya kijamii na jamii katika awamu ya kutunga. Kwa bahati mbaya, kama katika kisa cha Kaunti ya Isiolo, kulikuwa na kufuatilia finyu au hakukuwa na kufuatilia kokote na watu wale wale baada ya LAP kuzinduliwa, jambo ambalo limesababisha wengine wao kuona kuwa wameachwa nje. Hakikisha kuwa unazungumza na washika dau wakati wote wa utekelazaji.*

## 4.2 Kuhakikisha LAP inafanya kazi

### Tengeneza kazi mpango ya mwaka

LAP itabainisha ToC, kitu kinachoelezea lengo la LAP na matokeo ya haraka na ya muda na jinsi itakavyoafikia malengo yaliyotajwa. Kila mwaka, LPN iliyo na wajibu wa kutekeleza LAP lazima itunge kazi mpango inayoainisha matokeo na shughuli za namna itakavyofanya kazi ili kuafikia malengo na matokeo. Hatua ya kutunga ToC inapatikana katika Sehemu 3.2. Tazama Sura ya Tano kupata maelezo ya kina ya jinsi ya kutengeneza matokeo, shughuli na vibainishi. Kielelezo cha kazi mpango ya mwaka kinapatikana katika Kiambatisho E.

Kila shughuli inayofanywa sharti iwe na malengo yenye sifa za SMART (mahsusi, kupimika, kuafikika, inayofaa na kufanyika ndani ya mda fulani) ambayo inaweza kurejelewa mwishoni mwa mwaka. Vidokezo vya kuandaa kazi mpango ya mwaka:

- *Shughuli zote sharti zitekelezwe kwa kutumia rasilmali zilizoko.*
- *Shughui zote sharti ziainishwe katika ufinyu wa fedha, ufundi, itifaki au vikwazo vingine.*
- *Athari zote za shughuli sharti ziwe za kupimika na zifanye kazi kuelekea katika kuafikia matokeo.*
- *Kila shughuli sharti ihusishwe na taasisi au shirika, na lazima wakubali kuwajibika katika utekelezaji.*
- *Ni heri kuorodhesha shughuli chache ambazo zinaweza kukamilishwa kwa uzuri wa kiwango cha juu, badala ya shughuli nyingi ambazo hazina rasimali za kifedha au kibinadamu za kutosha.*
- *Kazi mpango ya kila mwaka sharti iandikwe wakati huo huo ambapo mazungumzo kuhusu rasilmali za kifedha na bajeti yanafanyika katika kiwango cha mtaa na kiwango cha kitaifa ili kuweza kuambatanisha shughuli katika mipango ya serikali na misururu ya bajeti.*
- *Kazi mpango sharti itaje msaada wa ziada wowote wa kiufundi unaohitajika ama ufahamu wa mapengo yanayohitaji kujazwa.*

### Tambua sera za ziada zinazosaidia LAP

Katika awamu ya kuandika, jopo kazi litakuwa limeainisha sheria na mapengo yaliyopo. Pamoja na kuweka LAP katika sheria ya mtaa, huenda pakawa na sera za ziada zinazohitajika kuidhinishwa ili kuwezesha utendaji kazi wa shughuli tofauti tofauti zilizo katika LAP. Baadhi ya sera hizi zitapatikana katika kiwango cha kitaifa, zinazoonyesha umuhimu wa kuhusisha wawakilishi wa kitaifa katika kila kiwango cha uandishi. Utekelezwaji wa LAP unaweza kuanza hata sera hizi zote zisipokuwa zimeundwa. Hata hivyo, lazima LPN iendelee kutetea mabadiliko ya sera katika sehemu zinazohitaji. Katika visa vingine, sera ama sheria huenda tayari ikawepo, lakini haitekelezwi ipasavyo; LPN sharti ipiganie utekelezwaji wake.

Baadhi ya mifano ni pamoja na:

- *Sheria za taasisi za kielimu.*
- *Ulinzi wa kijamii au ulinzi ulioshehеniwa katika misingi ya kijamii.*
- *Sera za uchumi-jamii zilizo jumuishi, ikiwa pamoja na ajira, afya, elimu.*
- *Ugatuzi au kupeleka sera mashinani.*
- *Upataji wa haki, ikiwa pamoja na mtindo mbadala wa kusuluhisha migogoro.*
- *Usajili wa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali.*
- *Sera za kupigana dhidi ya ufisadi.*
- *Sera za amani na mshikamano.*

***Mfano: Mfumo wa Kaunti ya Mombasa wa Ushirikiano wa Wanawake Katika Maendelo (CWID) na uundaji wa mwitiko wa kijinsia wa Onyo za Mapema na Majibu ya Mapema (EWER)***

*CBO ya Mombasa, CWID, ilionyesha kuwa hakukuwa na mfumo katika Kaunti ya Mombasa kujibu dalili za mapema za itikadi kali. Aidha, huku dalili za hatari zikiwa zinajulikana vyema miongoni mwa washirika wa P/CVE, jamii ilikuwa na ufahamu mdogo. CWID, kwa kushirikiana na serikali ya Kaunti ya Mombasa, Afisi ya Kaunti ya Mombasa na watalaamu wa kiufundi, walianzisha mchakato wa kuandika mfumo wenye hisia za kijinsia wa EWER. Mfumo wa EWER uliwekwa katika himaya ya CAP ya Mombasa lakini unafanya kazi kama sera ya kusaidia katika utekelezaji wa CAP.*

## 4.3 Kufadhili LAP

Ni muhimu kutambua wakati wa awamu ya kutunga kuwa rasilmali ni haba na kwamba matendo ya LAP lazima yawekwe katika rasilmali za kifedha zilizoko kadri iwezekanavyo. Jambo hili haliongezei nguvu mbinu za ufadhili za LAP lakini pia husaidia kuiambatanisha katika vipaumbele vya sera za ufadhili zilizoko. Njia za ufadhili zilizoko zinaweza kugawanywa katika makundi manne tofauti: kutumia kikamilifu rasilmali zilizoko, mitandao na miundo, kutumia fedha za mitaa na za kitaifa, kutafuta msaada wa mashirika ya kibinafsi, na kupata fedha za wafadhili ama CSO.

***Mfano: Youth Bila Noma (YBN) na Matumizi ya pesa za ugatuzi na kuzungumza na sekta ya kibinafsi***

*Ukosefu wa kazi miongoni mwa vijana, matumizi ya dawa za kulevya na usajili katika genge la majambazi ni changamoto zinazokabili vijana wa mji katika Kaunti ya Nakuru. Huku ikijulikana kuwa masuala haya hayahusiani moja kwa moja na itikadi kali za ghasia, yanasababisha kuwepo kwa hali ambamo vijana wanavutiwa zaidi na michakato inayopinga serikali na kupinga jamii. YBN, CBO inayoongozwa na vijana, inafanya kazi na vijana wa Nakuru ili kuhamasisha watu kuhusu masuala haya na kufanya maelekezo kutoka kwa wenza na kutoa stadi za kazi kwa vijana walio katika hatari. YBN imesaidia baadhi ya makundi ya vijana kujisajili kirasmi na kuwasaidia katika kufanya maombi ya ruzuku na mikopo kutoka kwa serikali. YBN pia imesaidia kuunganisha vijana walio katika hatari na biashara za mitaani ili kupata nafasi za kufunzwa kazi kwa afisi kadhaa za serikali ili kupata nafasi za kazi. YBN pia imewezesha kandarasi baina ya vituo vya polisi wa mtaa na moja kati ya makundi ya vijana ili kupaka rangi kuta za kituo.*

## Tumia kikamilifu rasilmali, mitandao, miundo iliyopo

Hata kwa bajeti ndogo, serikali za mitaa na mashirika ya kijamii bado yana rasilmali nyingi katika hali ya miundo mbinu, maunganiko na mitandao. Msaada wa ndani kwa ndani labda ndio ulio rahisi kupata na huenda ukawa wa kutumika na endelevu zaidi. Washikadau wa serikali na wasio wa serikali wanaweza kusaidia utekelezaji wa LAP kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja kwa kutoa msaada wa ndani kwa ndani kwa kutoa fedha ama kuchukua shughuli katika LAP na kuifadhili moja kwa moja. Ripoti na mafunzo ya hapa yanaweza kutolewa kwa washikadau wengine, wakiwa pamoja na jamii na serikali ya kitaifa na serikali ya kaunti, kupitia kwa LPN. Baadhi ya mifano ni pamoja na:

- *Kuwa mwenyeji wa hafla katika nafasi zinazotolewa na wahusika wa serikali ama wasiokuwa wa serikali kwa mfano, kumbi za serikali, afisi za CSO, vituo vya vijana, na mijengo ya kielimu ama ya kidini.*
- *Kutoa huduma za upishi.*
- *Rasilmali za uchapishaji.*
- *Kutoa msaada wa vyombo vya habari, pamoja na mitandao ya kijamii.*
- *Kutumia majukwaa ya mitandao kama vile Zoom, Survey Monkey, Skype, WhatsApp.*
- *Kutumia mitandao iliyopo, kama vile mpango wa kijamii wa usalama, mashirika ya kidini, makundi ya kina mama, makundi ya vijana.*
- *Kutoa msaada wa usafiri na taratibu, kama vile mabasi, magari ya kuzoa taka, vyombo vya sauti.*
- *Kutafuta taratibu za kujitolea miongoni mwa vijana.*
- *Kutolipisha kwa kushiriki katika hafla na shughuli.*

## Fikia bajeti na fedha za serikali ya kitaifa na ya kaunti

Ukiwa na uungwaji mkono wa wanasiasa, serikali zote mbili za mtaa na kitaifa zinaweza kuweka vipaumbele vya LAP katika mipango ya kisekta iliyoko, kama vile mipango ya maendeleo na ugatuzi. Pamoja na kujumuisha vipaumbele vya LAP katika mipango mingine mikubwa, serikali za mtaa sharti zihakikishe kuwa imepangwa na kutengewa fedha katika bajeti za kila mwaka. Mara nyingi pia kuna fedha za kitaifa zinazogatuliwa. LPN inafaa kuangalia sheria zilizoko zinazoongoza mahusiano ya ushirikiano baina ya serikali tofauti, ikiwa pamoja na ufadhili na bajeti. Kwa mfano:

- *Serikali za mtaa zinaweza kupanga na kutengeneza bajeti zinazohusiana na shughuli za P/CVE, mradi tu ziwe zimejumuishwa katika mipango yao ya maendeleo na kuidhinishwa na mabunge yao ya nyumbani katika michakato ya kutengeneza bajeti.*
- *Serikali za mtaa zinaweza kuzungumza na idara husika za serikali kuu wakati wa kupangia fedha katika bajeti ili zielekezwe kwa shughuli za LAP. Kimsingi, hii itahusu kuzungumza na wizara ya ugatuzi; itaweza kujumuisha huduma za kiasili za usalama.*
- *Serikali za mtaa pamoja na washirika wa utekelezaji wanaweza kufikia fedha zilizogatuliwa au mipango ya ruzuku kwa ajili ya shughuli za LAP inayoingiana na malengo ya ruzuku. Kwa mfano, CSO inaweza kufanya kazi na makundi ya vijana kwa kulenga watu walio katika hatari kubwa ili kuongeza uwezo wao wa kupata ruzuku ndogo kwa maendeleo ya kiuchumi au kuendeleza stadi za kazi.*

- *Serikali za mtaa zinaweza kufikia mipango iliyoko na ambayo tayari imefadhiliwa – kama vile mipango ya Elimu na Mafunzo ya Kiufundi (TVET) – ili kulenga watu walio katika hatari au kuongezea mafunzo yaweze kupatikana kwa urahisi zaidi au ya kufaa zaidi. Kwa mfano, iwapo kuna sekta kubwa ya utalii mtaani, huenda ukataka kuongeza stadi za upishi au lugha ya kigeni, badala ya stadi zilizozoeleka kama vile uvuvi katika kituo cha TVET.*

- *Serikali za mtaa zinaweza pia kuangalia mipango mingine ya ufadhili ambayo itasaidia kuboresha jamii huku ikisaidia kuchangia kwa malengo na makusudi ya LAP. Kwa mfano, serikali nyingi ziko na mipango ya kukarabati vituo vya polisi, kuanzisha vituo vya vijana au kuimarisha nafasi za sanaa na utamaduni.*

*Katika kaunti za Kenya zinazopakana na Somalia, serikali za kaunti zimesaidia Polisi wa Kitaifa wa Akiba (NPRs) kwa msaada wa usafiri na utoaji wa fedha kidogo za matumizi. NPR ni kiungo cha Polisi wa Kitaifa na kinajumuisha watu waliosajiliwa kutoka mtaani. NPR wamechangia kwa kiasi kikubwa katika uzuiaji wa ghasia katika baadhi ya kaunti na kujaza katika mapengo ya usalama.*

## Fanya ushirikiano na sekta ya kibinafsi

Inawezekana kutengeneza ushirikiano na sekta ya kibinafsi ili kuchanga pesa za shughuli za LAP. Jambo hili linahitaji uwezo mkubwa wa kutumia stadi kwa niaba ya serikali ya mtaa ama washirika wa utekelezaji wa CSO ili kunadi fursa kama kitu kilicho na manufaa kwa wote. Nafasi za N/CVE zinaweza kutumiwa, hususan pale ambapo VE imeonekana kuwa inayodhuru biashara za mtaa. Kuna tahadhari ama hatari inayohitajika kuangaliwa wakati wa kutumia njia hii ya kufadhili CAPs: biashara huenda zikalengwa na watu wenye misimamo mikali kwa kuunga mkono juhudi za P/CVE na kujaribu kuwadunisha na kuwaharibia sifa. Hata hivyo, hii ni hazina ambayo haijatumika katika ufadhili wa kinyumbani wa P/CVE nchini Kenya na kwingineko. Ingawa huenda kukawa na mifano michache ya ushirikiano kati ya umma na sekta za kibinafsi kwa mambo ya shughuli mahsusi za CVE, serikali za mtaa zinaweza kutafuta rasilmali kutoka kwa sekta zingine za kuzuia ghasia.[14]

*Katika Kaunti ya Kwale, Base Titanium (kampuni ya kuchimba madini katika sehemu hiyo) imekuwa ikisaidia shughuli za vijana, ikiwa pamoja na, ingawa sio tu biashara ndogo ndogo na nafasi ya mazoezi ya kazi kwa vijana. Kando na mfano huu, biashara zingine kadhaa katika Kaskazini Mashariki mwa Kenya zimekuwa zikisaidia michakato ya kutafuta amani kama vile midahalo na mazungumzo miongoni mwa jamii tofauti tofauti hasa katika Kaskazini Mashariki mwa Kenya. Jambo hili lilihusisha ingawa sio tu, misaada ya vyakula na mahitaji mengine wakati wa michakato ya kutafuta mani.*

## Kupata fedha za ufadhili kupitia kuandika mapendekezo na kufanya michango

Mpaka sasa, baadhi ya vianzo vikubwa vya fedha za shughuli za LAPs na P/CVE zinatoka kwa wafadhili. Hata hivyo, huku hizi fedha zikiweza kutumika katika uzinduzi wa LAP, huenda zisiweze kuwepo hatimaye, na mara nyingi wafadhili wataamua ni shughuli zipi za kutekelezwa bila kujali vipaumbele vya jamii. Mabalozi na mashirika ya kimataifa aghalabu yataitisha mapendekezo katika tovuti zao, na serikali za mtaa na mashirika ya kutetea haki yanaweza kuwafikia moja kwa moja kuomba msaada. Inaweza kuwa muhimu kuendea serikali ikielekea kufika mwisho wa mwaka wa matumizi ya fedha watakapokuwa wanatafuta kujua namna watakavyopangia fedha zao za ziada katika bajeti. Wafadhili kwa kawaida watakuwa na sehemu za kipaumbele ambazo unafaa kuzijua mapema kabla ya kutoa mapendekezo yako.

Yaliyomo —

## 4.4 Kusahihisha na kurekebisha LAP

Hata kama mji wako hauna LAP kamili, ni muhimu kuhakiki stakbadhi zote na miundo kila mwaka ili kuhakikisha kuwa mafunzo yaliyopatikana yanajumuishwa na kwamba LAP inatoa nafasi ya kuitikia mabadiliko katika muktadha.

### Kadiria athari na kuunda kazi mpango mpya

Kila mwaka, sharti LPN iandae kongamano kuhakiki utekelezwaji wa LAP kufikia wakati huo na kuhalalisha kazi mpango ya mwaka utakaofuata. Uhakiki wa kila mwaka unaweza kufanywa na jopo ndogo la kazi ama mtu kabla ya kongamano. Vilevile, kazi mpango inaweza pia kuandikwa mapema kwa kutumia jopo ndogo la kazi ama kwa kuwa na kila jopo ndogo la kazi la kila maudhui kuwasilisha maoni yao mapema. Ni muhimu kuelewa athari pana ya LAP kufikia wakati huo. LPN sharti pia iangazie athari za LAP za moja kwa moja na zile zisizokuwa za moja kwa moja na kujaribu kuelewa kama kila kitu kilienda kulingana na mpango na jinsi ambavyo LAP ilikabiliana na changamoto.

### Sahihisha miundo ya ushirikishi

Kila mwaka, viongozi wa LPN sharti wahakiki uanachama na kuongeza ama kuondoa taasisi na mashirika ama kurekebisha anwani zao. Kila badiliko lazima lifanywe kwa uwazi na kwa njia ya kupata ushauri kwa kushirikiana na uanachama wote. Sharti LPN iendelee kuhakikisha kuwa wanawake, vijana na makundi yaliyotengwa yanawakilishwa katika nafasi za uongozi kwa njia inayopita uanachama wa kufurahisha wahusika tu. Baadhi ya mifano ya uanachama inaweza kuzingatia:

- *Kustaafu ama mabadiliko katika uajiri wa wafanyakazi.*
- *Mabadiliko katika masuala ya kipaubele ama mihimili inataka washikadau wa kiufundi wapya kuongezwa.*
- *Kila shirika linafanya uamuzi wa kimkakati ili kufanya kazi tena na mada husika za P/CVE.*
- *Mashirika mapya yanaundwa (kupitia michakato ya kisheria, sera ama uongozi), ama shirika lililoko kuchukua kazi husika ya P/CVE.*
- *Mabadiliko katika sehemu ya kijiografia ya kufikiwa na LAP, kama vile sehemu mpya yenye hitaji ama mabadiliko katika sehemu ya uwakilishi ya kisiasa.*
- *Chagamoto zinazotokana na kufanya kazi na shirika fulani ama mtu binafsi*.*

*Iwapo masuala yataibuka na shirika ama mtu binafsi aulizwe kutoka LPN, jambo hili sharti lifuate njia ya uwazi. Ni sharti lifanywe kwa mujibu wa sheria za hulka za kikazi ama ToR zilizokubalika katika awamu ya kuandika pamoja na mgao wa kazi na majukumu katika LPN.

### Angalia upya makadirio ya hatari (kila mwaka) na LAP (kama inavyotakikana)

Kama tathmini yako ya mtaani ya hatari ilipata kiwango cha chini cha hatari kutoka kwa VE na mji wako ukaamua kutotunga LAP, basi jopo kazi lako sharti liitishe kikao tena ili kubadilisha makadirio ya hatari ya mtaa. Iwapo kiwango cha hatari kitabaki chini, hapatakuwa na haja ya kuchukua hatua ya ziada; hata hivyo, kama kiwango cha hatari kimeongezeka, jopo kazi linaweza kuamua kuanza mchakato wa kutunga LAP.

Kila mji ulio na LAP sharti uhakiki na kubadilisha ili kujumuisha mafunzo yaliyopatikana, mabadiliko ya muktadha na mabadiliko yoyote katika miundo ya ushirikishi ama mipango ya utekelezwaji. Masafa ya kazi hii na rasilmali zitakazohitajika vitategemea na LAP yako binafsi. Kwa mfano, huenda ikatosha kufanya kongamano la mwaka la kuhakiki na kusifanywe mabadiliko yoyote ya maana. Hata hivyo, hasa iwapo imechukua miaka kadhaa tangu stakbadhi kutungwa, LAP huenda ikahitaji mchakato mkubwa zaidi wa kuhakiki, suala linalofanya mabadiliko makubwa kufanywa ama kuundwa stakbadhi mpya kabisa.

Zana utakazotumia ni pamoja na:

- *Makundi lengwa ya mijadala.*
- *Mahojiano ya watoa taarifa muhimu.*
- *Usahihishaji wa utafiti mpya, taarifa mpya na ama stakbadhi za miradi.*
- *Uchunguzi lengwa wa mtandaoni na usiokuwa wa mtandaoni.*
- *Mikutano ya kijamii.*
- *Kongamano la kila mwaka na majopo kazi pamoja na mashirika ya ushirikishi na utekelezaji.*

Sharti uhakiki ulenge kupambanua kile ambacho kimetekelezwa na kile ambacho, iwapo pana chochote, kilichobadilika katika mazingira unamofanyia kazi. Uhakiki unaweza pia kutathmini namna ya kuboresha utelekezaji. Kama unaangazia tathmini kubwa kwa kusudi la kufanya mabadiliko makubwa katika stakbadhi yako uliyofanyia marekebisho, unaweza kuangalia sababu kama hizi zilizoorodheshwa hapa chini. Tathmini inaweza kuwa yenye misingi ya kuchukua hatua, kukiwa na mapendekezo ili kujumuisha katika stakbadhi iliyorekebishwa kwa mifano ifuatayo:

- *Ufahamu na ufaafu wa LAP.*
- *Kiwango cha washikadau kuingiliana na LAP.*
- *Ushirikiano na ushirikishi wa washikadau.*
- *Mifumo ya M&E.*
- *Hali ya utekelezaji wa shughuli.*
- *Uwezo wa mapengo (kiufundi).*
- *Upataji wa rasilmali za kujaza mapengo na ushirikishi (kifedha).*

Yaliyomo —

# Sura ya Tano

## Ufuatiliaji na Tathmini ya LAP

Ufuatiliaji na tathmini ya LAP ni sehemu ambatanishi ya kazi nzima ya LAP. Hii inawezesha washikadau kuchunguza maendeleo ya utekelezaji, kuatambua mapengo yoyote yanayohitaji kushughulikiwa na kutambua mafunzo ya kuongoza mabadiliko ya baadaye ama utekelezwaji wa jumla.

**Baada ya kusoma sura hii, hakikisha kuwa unaelewa:**


1. Umuhimu wa ufuatiliaji na tathmini (M&E) katika utekelezaji wa LAP.
2. Mchakato wa kufanya masuala ya M&E.
3. Namna ya kuandaa majukumu na wajibu wa kufanya kazi ya LAP M&E.

## 5.1 Kuanzisha ToC


ToC inaelezea uhusiano kati ya shughuli na matokeo yanayotarajiwa. Jambo hili linaweza kuainishwa kama mchakato wa mabadiliko katika chati ya mtiririko, ambayo wakati mwingine inaitwa kielelezo cha mantiki. ToC inayopendekezwa na SCN ina viwango sita. Viwango vitatu vya juu vinainisha mabadiliko unayotarajia kutendeka, na viwango vitatu vya chini vinaonyesha vitendo ambavyo kupitia kwavyo haya mabadiliko yatapatikana. ToCs zinapangwa katika utaratibu huu ili kukumotisha ufanye kazi ukirudi nyuma, ukianza na lengo kuu. Jambo hili linahakikisha kuangazia mabadiliko unayotaka yafanyike badala ya kuangazia vitu ambavyo LAP hufanya.

| | |
|---|---|
| **LENGO** | Lengo kuu la mradi wa muda mrefu na mabadiliko ya kiwango cha juu ambayo inakusudia kuchangia, lakini haiwezi kufanikiwa peke yake. |
| **MAZAO YA KATI** | Matokeo ya muda wa kati wa mradi ambao unatarajiwa kupatikana mwishoni mwa kipindi cha kutuliza. kawaida hujimuisha mabadiliko ya tabia, mazoezi na utendaji. |
| **MAZAO YA HAPO HAPO** | Athari za muda mfupi za mradi kwa walengwa wake. Hizi zinajumuisha mabadiliko katika uwezo kama vile kuongezeka kwa maarifa, ujuzi, ufahamu, mtazamo au ufikiaji |
| **MAZAO** | Bidhaa au huduma za moja kwa moja zinazotolewa katika kiwango cha mradi na utekelezaji wa shughuli. Matokeo husababisha matokeo, lakini sio mabadiliko yanayotarajiwa kutokea. |
| **SHUGHULI** | Mradi gani hufanya kweli. Hizi ni hatua zilizochukuliwa au kazi iliyofanywa kupitia ambayo pembejeo zinageuzwa kuwa matokeo ya mradi. |
| **PAMBEJEO** | Rasilimali watu, fedha, shirika na jamii zinahitajika kutekeleza mradi. |

ToCs mara nyingi hupangwa katika muundo wa piramidi. Muundo huu unasaidia kuonyesha mantiki ya kisababishi–na-matokeo ili kubainisha aina hii ya mfumo. Ili kusonga juu katika kielelezo cha mantiki kuelekea kwenye lengo, kikundi cha viungo vya kiwango cha chini lazima kwanza vimalizike au kuafikiwa. Huku ikiwa kwamba LAP sharti iwe na lengo moja kuu, idadi ya viungo vipande katika kila kiwango mara nyingi huongezeka.




ToC inaweza kuchukua muundo rahisi kama huu pale juu, ama inaweza kuwa changamano kama mchoro ulio hapa chini. Ni muhimu kukumbuka kwamba katika mazingira changamano, uhusiano kati ya kila kiwango cha ToC kinafanya kazi kwa uwezo mkubwa na mara nyingi kwa kutegemea nadharia-tete nyingi. Hii ni kwa sababu ni nadra sana kupata mabadiliko katika mtindo wa laini nyoofu. Kielelezo kama hiki kinaweza kuonekana katika mfano wa hapa chini, unaowakilisha mradi wa SCN uliojumuisha utengenezaji wa LAP na LPN/CAT huko Kumanovo, Macedonia Kaskazini.




Sharti ToC iambatane na maelezo yanayoonyesha uhusiano au mishale kati ya kila kiungo cha kielelezo mantiki. Ni lazima ichote kutoka katika taarifa iliyokusanywa wakati wa tathmini ya hali na ni lazima ianze kwa kuelezea kwa kifupi muktadha wa LAP na walengwa wake. Maelezo ya ToC sharti yatafute nadharia-tete zinazobainisha kila unganiko ama mshale katika kielelezo mantiki, pale panapowezekana kutoa ushahidi wa kuchangia kila dai kwamba kiungo kimoja kitasababisha kuwepo kwa kingine.

Naharia-tete ya ToC ni zana ya msaada kwa kuunda kila dhana na kuunganisha na hali kwa badiliko unalotaka kuwa nalo. Zana hii huandikwa kwa kutumia tarifa: 'Ikiwa ...................., basi .......... kwa sababu............'.

## Kuelezea lengo lako

Malengo ni taarifa pana zinazoonyesha 'kwa nini' ya muradi wako. Yanaelezea badiliko la mwisho katika hali ama wema unaotaka walengwa wako kupata. Lengo zuri mara nyingi litawasilisha kusudi la tamanio kubwa, la muda mrefu ambalo halitaweza kuafikiwa ndani ya muda wa LAP yako. Kwa sababu hii, inawezekana kwamba baadhi ya sababu zitachangia katika ufaulishaji au kutofanikiwa kwa lengo la mwisho, nyingi ya hizo huenda zikawa nje ya uwezo wako. Hata hivyo, lengo lolote lile unalochagua, lazima uhakikishe kuwa ni kitu ambacho muradi wako unaweza kuchangia kwa njia ya kihalisia. Hata hivyo, tofauti na mavuno na matokeo, hayahitaji kuwa ya kupimika.

***Mfano wa lengo:*** *Ongezeko la ustahimilivu wa wanachama wa jamii ya VE kule Kumanovo*

### Kuandaa matokeo ya kati

*Matokeo ya kati yanachangia lengo la LAP na ni matokeo ya kiwango cha juu ambayo yanaweza kuafikiwa kwa njia ya moja kwa moja kupitia kwa shughuli unazofanya. Lazima yaonyeshe mabaliliko unayonuia kapata, badala ya kuelezea shughuli ulizofanya. Hakikisha kuwa malengo yako yanazingatia akronimu za **SMART**, ama angalau yahusishe nyingi ya kanuni zake.*

| | |
|---|---|
| **Lenga ndipo** | Je, badiliko linalotarajiwa limeelezwa? |
| **Kupimika** | Je, badiliko linaweza kupimika? |
| **Ufaafu** | Lengo linaingiana na kusudi unalojaribu kuafikia, na litachangia katika uafikiaji wake? |
| **Uhalisia** | Je, lengo linaweza kuafikiwa kwa kutumia rasilmali zilizoko kwa muradi wako? |
| **Kiwakati** | Lengo linaweza kuafikiwa ndani ya wakati uliopo wa muradi? |

*Hapa chini pana baadhi ya malengo kutoka kwa muradi wa ushirikiano wa kibinafsi/umma wa SCN kule London, Uingereza. Inapendekezwa kuwa usiunde zaidi ya matokeo ya kati mawili hadi matano kwa lengo lako la mwisho.*

***Lengo 1:*** *Ongezeko la shawishiko la kampuni za kibinafsi kuunda ushirikiano endelevu na CSOs katika sekta ya P/CVE.*

***Lengo 2:*** *Ongezeko la upataji wa rasilmali zinazotolewa na sekta ya kibinafsi moja kwa moja na wahusika wanaofanya kazi katika sekta ya P/CVE.*

### Kuandika taarifa za matokeo

*Kuandika matokeo yenye athari, na ya kupimika kutoka mwanzoni ni muhimu iwapo unatazamia hatimaye kukadiria juhudi zako. Kuhakikisha kuwa unaandaa taarifa za matokeo ambazo zinaeleza waziwazi mabadiliko unayotaka yatendeke, unahitajika kujumuisha ujumbe wa kitu gani kitabadilika, njia ambayo mabadiliko hayo yatafuata, nani ataathirika na mabadiliko hayo na ni wapi mabadiliko hayo yatatendeka. Njia moja ya kuandika matokeo inaweza kupatikana katika jedwali la hapa chini. Hizi taarifa shartti ziandikwe katika wakati uliopita, kwa misingi kuwa zinanuiwa tu kuonyesha mabadiliko mwishoni mwa muradi. Ni lazima ujumuishe badiliko moja tu katika kila tokeo.*[15]

| Mkondo | Nini | Nani | Wapi |
|---|---|---|---|
| Kuboreka | ufahamu wa kuripoti huduma za uhalifu wa chuki | miongoni mwa makundi madogo | katika jamii zilizochaguLiwa katika mji X |
| Kuongezeka | Imani katika washikadau wa kuzuia wa LAP na VE | miongoni mwa jamii lengwa | katika eneo Y |
| Kupunguka | kuwa katika hatari katoka kwa maoni ya wenye misimamo mikali | miongoni mwa vijana walio katika hatari | katika wadi Z |
| Kuongezeka | kuunga mkono ajenda ya VE ya kuzuia | miongoni mwa maafisa wa kaunti | katika wilaya Y |
| Kuongezeka | ufahamu na stadi za VE | ya wanachama wa jopo kazi wa LAP | katika nchi X |

## Kuandika taarifa za mazao

Taarifa za mazao zinaoonysha huduma ama matokeo ambayo muradi wako ama LAP inatoa kwa walengwa wake. Taarifa hizi lazima zijuimuishe habari kuhusu zao gani ama huduma iliyoafikiwa, katika somo gani na kwa nani.[16] Njia moja ya kuandika mazao inaweza kupatikana katika jedwali la hapa chini.

| Nini | Kitenzi | Somo | Nani |
|---|---|---|---|
| Mafunzo | imetolewa | katika ufahamu wa elimu na kupata mipango ya serikali ya ufadhili | kwa vijana-walio-nje ya shule katika nchi Y |
| Zoezi bora la kuongoza | sambazwa | katika ufundishaji wa stadi za kidijitali za uraia | kwa vijana wafanyakazi katika mji Z |
| Msaada wa kiufundi | Imetolewa | katika kufanya kazi na makundi ya kijamii ya mtaani katika upangaji wa matukio | kwa wafanyakazi wa serikali ya mtaa katika kaunti X |
| Fursa za maunganiko | imepangwa | kuunganisha serikali ya mtaa na mashirika ya kijamii | kwa CSOs katika mji X na kaunti Y |

## 5.2 Kuunda Viashiria

Viashiria ni vibadili vinavyopimika vinavyotarajiwa kubadilika kutoka kwa thamani moja mwanzoni mwa muradi kwa nyingine mwishoni mwake. Vinaweza kuwa vya kihisibati na visvyo vya kihisibati na lazima kutoa mbinu rahisi na za kutegemewa kwa kutathmini iwapo viungo vya ToC yako vimeafikiwa.

Kuunda kiashiria kinachoweza kupima matokeo, ni lazima ujumuishe: kipengee cha kupima, kama vile tarakimu ama asilimia; nani anapimwa; na ni kitu gani kitakachopimwa.

## Viashiria vya kihisibati

Kwa kawaida, hisibati haina mapendeleo na hupima idadi ama vipimo vya kitu. Kitengo cha kupima katika viashiria hivi kwa kawaida ni tarakimu, asilimia ama sehemu.[17]

| Kitengo cha kupima | Kitengo cha uchanganuzi | Muktadha |
|---|---|---|
| # | ya maafisa wa manispaa | kukamilisha vipindi vyote vinne vya warsha ya mpango kazi wa mtaa |
| % | ya vijana waliopata mafunzo | nani anaripoti mabadiliko katika usambazaji wa vianzo vya habari wanazopata mtandaoni baada ya kushiriki katika warsha shuleni |
| % | ya walimu | nani anapokea gredi ya ufua dafu katika mtihani katika kuwa na mazungumzo magumu katika darasa na vijana walio katika hatari |
| **Kiwango** | ya wanawake kwa wanaume | katika nafasi za kutoa maamuzi katika kiwango cha mtaa |

## Viashiria visivyokuwa vya kihisibati

Viashiria visivyokuwa vya kihisibati ni vya mapendeleo na kwa kawaida hunasa deta kutokana na tajiriba, hisia na utendaji kazi. Mbinu kama vile vipimo, uchanganuzi wa yaliyomo ama uchunguzi wa kitaratibu waweza kusaidia kuhesabu deta.[18]

| Kitengo cha kupima | Kitengo cha uchanganuzi | Muktadha |
|---|---|---|
| % | ya maoni yaliyotolewa na watumiaji | iliyo chanya katika uchanganuzi wa maoni ya siri yaliyotolewa kama mwitiko kwa video ama mtandao wa You Tube |
| Kiwango wastani cha kutosheka (kwa pointi 7 katika kipimo cha likert) | ya wafanyakazi wa CSO | pamoja na maelezo ya mafunzo ya kuzuia yaliyotolewa wakati wa warsha |
| % | ya walimu | wanaoripoti kuongezeka kwa imani katika kuwepo kwa mijadala migumu darasani na vijana walio katika hatari |
| **Uzuri** | wa LAP | ulioundwa na wanachama wa LPN |
| | | Uzuri wa LAP unapimika kupitia:<br>(1) Kufikiria mazoezi bora<br>(2) Kuweka sambamba na mahitaji ya mtaa yaliyotambulika, sababu za hatari na mkakati wa kitaifa<br>(3) Ujumuishaji wa makundi katika jamii ya mtaani<br>(4) Uwezekano wa mpango kazi<br>(5) Muonyesho wa maono na mpango wa muda mrefu. |

## Misingi na malengo

Kukusanya deta ya msingi kunakupatia mahali pa kurejelea dhidi ya hatua zilizopigwa katika upatikanaji wa mazao, matokeo na makusudi. Deta yako ya msingi sharti irekodiwe kwa kutumia kiwango hicho hicho cha kupimia kutambuliwa katika kiashiria na, panapofaa, kutengwa katika jinsia, kabila, nk.


Malengo yanatambua thamani mahsusi unayotaka kuona kwa moja kati ya viashiria vyako kufikia mwisho wa muradi. Malengo sharti yawe yenye matamanio makuu, lakini yanayoweza kuafikiwa, na ni bora kutengenezwa baada ya kukusanya misingi. Baadhi ya mifano ya awali ya viashiria imeorodheshwa katika jedwali hapa chini.

| Kiashiria | Msingi | Lengo | Iliyopatiana |
|---|---|---|---|
| Kiwango cha wastani cha kutosheka (kwa pointi 7 katika kipimo cha likert) | NA | 5.0 | 5.9 |
| % ya walimu wanaopokea gredi ya kufuzu katika mtihani kuhusu kuwa na mazungumzo magumu darasani na vijana walio katika hatari | 51% | 70% | 78% |
| # ya maafisa wa manispaa kumaliza vipindi vyote vinne vya warsha ya mtaani kuhusu mpango kazi. | 0 | 120 | 117 |
| Kiwango cha wanawake dhidi ya wanaume katika nafasi ya uongozi katika serikali ya mtaa. | 1:4 | 1:2 | 1:2 |

## 5.3 Kukusanya deta za kupima kufaulu

Kukusanya deta inayotegemewa ni kitovu cha mpango wowote mzuri wa M&E, na kuna aina nyingi za zana zinazoweza kutumiwa kukusanya taarifa ambayo muradi wako unahitaji. Hali tata ya mpangilio wa P/CVE pia unaleta changamoto za ziada katika ukusanyaji wa deta. Katika hali zingine, kupata na kufikia hadhira lengwa huenda kukawa kugumu sana.

Ni muhimu kufikiria kuhusu aina za deta unayoweza utarajia kukusanya wakati wa kuandaa viashiria vyako. Mchoro ulio hapa chini unaonyesha njia tofauti zinazoweza kutumika kukusanyia deta. Zozote zile unazochagua inafaa kuwa kwa misingi ya uwezo wa M&E yako, na mfinyiko wowote wa mda ambao huenda ukawa nao. [19]




Asilia: Kutoka Marchant 2000

### Kujaza fomu

Kujaza fomu ni zana inayotumiwa sana na M&E. Inaweza kutumiwa kupata deta za kihisabati na zisizo za kihisabati. Mbinu hii kimsingi huuliza washiriki kutoa ripoti kuhusu demografia zao, hisia, ujasiri, ufahamu-ujasiri na hulka.[20] Ni muhimu hasa wakati wa muradi unaokuhitaji ukusanye taarifa za kulinganisha ambazo zinapatikana kwa urahisi kutoka kwa makundi makubwa ya watu na ambazo zinaweza kutumika katika kiwango cha mtu binafsi, kama vile washiriki katika warsha. Kujaza fomu kunaweza kufanywa kwa kuwapa washiriki maswali kwenye karatasi ama kuwatumia kwa njia ya kidijitali ukitumia majukwaa kama vile SurveyMonkey. Baadhi ya aina ya maswali yanayotumiwa katika ujazaji wa fomu yameelezwa hapa chini.

- **Maswali ya wazi:** Maswali ya wazi yanamruhusu mtu kujibu katika njia yoyote iliyo wazi.
- **Maswali funge:** Haya ni maswali yanayompa mshiriki uteuzi wa jibu kutoka kwa majibu mawili yaliyotolewa, kwa kawaida 'Ndiyo/La' ama 'Kweli/Urongo'.
- **Maswali yenye majibu kadhaa:** Ni aina ya maswali funge ambapo washiriki wanapewa majibu kadhaa na kuulizwa wachague moja.
- **Maswali ya visanduku:** Kama maswali ya majibu kadhaa, maswali ya visanduku yanampa mshiriki majibu mengi lakini humruhusu kuchagua majibu kadhaa kulingana na maamuzi yao.

Yaliyomo

- **Maswali ya aina ya Likert:** Haya hutumia kipimo cha kiakili na kwa kawaida hutumika kupima hisia na maoni. Maswali ya aina ya Likert hupangwa kwa msururu wa pointi 5-ama 7 yanayoainishwa kutoka kiwango kimoja cha hisia za mwisho hadi kingine, kwa mfano 'Ninakubaliana kabisa' hadi 'Kutokubaliana kabisa', huku pakiwa na msimamo wa kati.

- **Maswali ya kidaraja:** Maswali haya yanamruhusu mshiriki kuweka viwango ama kupanga orodho ya teuzi katika utaratibu maalum kulingana na wanavyoona.

Huku kujaza fomu kukiwasilisha zana muhimu ya M&E, mbinu hii ina upungufu kadhaa. Kujaza fomu kuna upungufu wa idadi ya maswali yanayoweza kutumika na huenda kusiwe na uwezo wa kuangazia masuala ambayo ni muhimu katika utekelezaji wa muradi. Hivyo hivyo, taarifa zilizoripotiwa na mtu binafsi sio za kutegemewa wakati wote kwa sababu zinaweza kuvurugwa kwa mapendeleo kutoka kwa washiriki na watafiti wenyewe.

## Kujaza fomu ya ufahamu

Kujaza fomu ya ufahamu ama mijarabu ni kategoria ndogo ya mbinu ya kujaza fomu inayopania kukusanya deta kwa njia isiyokuwa na mapendeleo kuhusu upatikaji wa ufahamu na inawezakuwa ya manufaa makubwa ya kudhihirisha athari ya miradi ya kujenga uwezo wa watu. Kufuatilia mabadiliko katika hulka za walionufaika na miradi kuleta changamoto ya mara kwa mara katika P/CVE ambazo ni vigumu kuzishinda. Kutokana na hayo, kuelewa jinsi ufahamu wa mtu na uwezo wake wa kuutumia huenda umebadilika kunachukua umuhimu wa ziada. Ukiunganisha na deta za kihisia, hii inaweza kusaidia kutengeneza uelewaji mzito wa athari ya muradi na kusaidia kuepukana na utegemezi mkubwa wa mabadiliko ya hulka yanayoripotiwa na mtu binafsi.

## Makundi lengwa

Mbinu hii ya kukusanya deta inajumuisha kufanya mikutano ya mijadala ya makundi madogo kati ya muwasilishaji na walengwa ama washikadau ili kutambua taarifa inayofaa muradi. Maswali yanoyoulizwa katika mijadala ya makundi lengwa kwa kiasi kikubwa yanaweza kugawanywa katika makundi mawili: maswali zalishi, ambayo ni pana na wazi; na maswali ya kutaka kujua zaidi, yanayonuia kupata majibu kwa ndani na kuzingatia vipengele vyenye umuhimu kwa wafanyakazi wa muradi. Makundi lengwa kwa njia kuu ni njia ya kukusanya deta isiyokuwa ya kihisabati ingawa njia za kihisabati pia zinaweza kutumiwa kupitia kwa maswali mahsusi na stakbadhi.

## Mahojiano

Kama ilivyo katika makundi lengwa, mahojiano yanategemea majadiliano kati ya anayehoji na mlengwa ama mshikadau ili kupata undani wa suala la muradi. Huku kukiwa na uhusiano mkubwa kati ya mbinu hizi mbili, kama utaratibu wa maswali na sababu kuwa zote kwa kiasi kikubwa zinanasa maoni yasiyokuwa ya kihisabati, pia kuna vipengele kadhaa vya utofauti. Mahojiano kwa kawaida yanahitaji muda mwingi zaidi na rasilmali ili kupanga, na kwa hivyo ni bora kutumika kwa mijadala na walengwa ama washikadau wakuu.

## Kutazama

Pia hujulikana kama somo la utazamaji. Hii ni moja kati ya mbinu za kimsingi zaidi zilizoko katika M&E na mara nyingi hutumika pamoja na mbinu zingine za kukusanya deta. Kutazama kunajumuisha wafanyakazi wa muradi kuangalia walengwa na kurekodi na kuchanganua yale wanayofanya.

## Matumizi ya mfano

Mifano sio zana ya kukusanya deta hasa, lakini ni kazi elezi ambayo inaweza kutoa tathmini ya kindani ya somo ama mada. Kwa kawaida inategemea taarifa iliyokusanywa kupitia kwa zana nyingi na kutumiwa kuchora taswira ya kindani kuhusu sehemu maalum ya muradi inayoweza kuzungumzia athari pana ya mchakato kwa jumla. Mifano mara nyingi huangazia kiungo kimoja cha uchanganuzi kama vile mtu binafsi, familia, jamii, eneo ama shirika.

Yaliyomo —

# Kiambatisho A –
## Faharasa

**Kwa makusudi ya chombo hiki cha zana, yafuatayo ni maelezo ya istilahi kuu, dhana na mafungu ya maneno yanayotumika kote katika chombo cha zana.**

Katika-hatari ama kuwa katika mazingira magumu: Hali za kijamii, kisiasa, kimawazo ama kiuchumi ambazo mtu binafsi ama kundi la watu hupitia na huenda zikafanya mtu huyo ama kundi la watu kuwa katika hatari ya kutiwa katika itikadi kali na kuelekea katika itikadi kali ya ghasia.

Mashirika yenye misingi ya kijamii (CBO): Mashirika ya mashinani ambayo yamesajiliwa katika mtaa kama makundi-ya-kujisaidia. Makundi ya mashinani, mashirika na miunganiko pia yanaitwa CBOs.

Jukwaa la Mazungumzo la Kijamii (CEF): Katika kaunti za Kenya, CEF ni muungano wa washikadau wa kiserikali na wasiokuwa wa kiserikali. Unawajibikia utekelezaji wa CAP. CEF inajadili vipaumbele vya utekelezaji wa CAP, ushirikishi, mafunzo ibuka na hoja za kuingilia kati. Muundo wa SCNs na LPN ni wa kulinganisha.

Kazi Mpango ya Kaunti (CAP): Kuna vizazi vitatu vya CAPs katika Kenya. Kizazi cha kwanza cha CAPs kiliundwa katika kaunti za pwani – hususan Kwale, Mombasa na Lamu – mwaka wa 2017. Ilikuwa mipango ya miaka mitano. Kizazi cha pili cha CAPs kiliundwa mwaka wa 2018 katika kaunti za pwani zilizosalia, kaunti za Kaskazini Mashariki zinazopakana na Somalia na kaunti zingine zilizo katika hatari kama vile Isiolo na Marsabit. CAPs hizi ziliundwa kutokana na ushauri kutoka kwa Kituo cha Kitaifa cha Kupambana na Ugaidi (NCTC). Kizazi cha mwisho (cha tatu) cha CAPs kiliundwa mwaka wa 2019 kufuatia Amri ya Rais. Ziliundwa kwa haraka, ndiyo maana wakati mwingine zinaitwa RCAPs. Zililenga zaidi sana mipango ya mwaka mmoja.

Muungano wa Mashirika ya Kijamii (CSO): Kwa jumla istilahi hii inarejelea mashirika na taasisi zinazofanya kazi kwa manufaa ya wananchi – ikiwa pamoja na miungano isiyokuwa rasmi, mashirika ya kutetea haki za wafanyakazi, wanaharakati, watoa misaada, taasisi za kidini, vyombo vya habari, kati ya mengine.

Kanuni za Kuongoza: Kanuni hii kwa jumla inarejelea imani, kaida na sifa zingine zinazoongoza maendeleo, utekelezaji na mabadilko ya LAPs. Wale ambao wamepewa jukumu la maendeleo na utekelezaji wa LAPs, ikiwa pamoja na taasisi, lazima wazingatie kanuni za kuwaongoza. Kuna makundi matatu ya kanuni za kuongoza: (a) vigezo vikuu vinavyoainisha mkakati wa LAP na muundo wa ushirikishi; (b) masharti ya mchakato na uongozi yanayoongoza mbinu za kuandika LAP na muundo wa ushirikishi; na (c) maeneo ya kipaumbele yanayobainisha makundi makuu ya maudhui ya kuingilia kati.

Viashiria: Hizi ni sifa ama masharti yanayolenga ndipo, yanaweza kuonekana, kuafikika, ya kiuhalisia, yanayopimika na kufanyika ndani ya muda fulani na ambazo zinaweza kutumiwa kuonyesha mabadiliko ama maendeleo. Kwa mfano: # ya shughuli za LAP ambazo serikali ya mtaa imejumuisha katika mpango wa kifedha.

Michango-ya-Bidhaa: Hizi ni rasilmali, za kifedha na zisizokuwa za kifedha, ambazo zimechangwa ili kusaidia katika utekekezaji wa LAP kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Kwa mfano, shirika linaweza kugharamia mafunzo ya wanachama wa LAP kwa kulipia mafunzo bila kutoa fedha moja kwa moja kwa LPN. Shirika linaweza pia kutuma mtaalamu kusaidia utekelezaji wa LPN.

| |
|---|
| Jopo Kazi la Muda: Hili ni jopo kazi lisilokuwa la kudumu ambalo limeundwa ili kuandika LAP. LAP ikishaundwa na kuhalalishwa, nafasi yake itachukuliwa na kikundi cha kudumu cha utekelezwaji, ambacho ni LPN. |
| Kiongozi mshirikishi wa Kuzuia: Mtu aliyeajiriwa na serikali ya mtaa na anawajibikia utelezaji wa LAP na ushirikishi wa LPN. |
| Mpango Kazi wa Mtaani (LAP): Huu ni mpango ama mkakati wa P/CVE wa eneo dogo la taifa (km. mji,jimbo, kaunti, mkoa) lililoundwa na serikali ya mtaa ili kusaidia katika ushirikishaji na washikadau wa mashirika yasiyokuwa ya serikali na jamii. |
| Ushirikiano Kati ya Serikali Kuu na Mtaa: Hii inajumuisha ushirikiano wima baina ya wahusika wanaofaa walio kwenye kiwango cha kitaifa na kiwango cha mtaa katika nchi fulani. Wahusika hawa wanaweza kuwa tofauti kutegemea na nchi na wanaweza kujumuisha serikali kuu, serikali ya mtaa, wataalamu wa kulinda sheria, wafanyakazi katika sekta ya afya na elimu pamoja na mashirika husika ya kutetea haki (CSOs), sekta ya kibinafsi, na watafiti.[21] |
| Muunganiko wa Mtaani wa Kuzuia (LPN): Hili ni shirika la wahusika wa serikali na wasio wa serikali wanaongoza utekelezaji wa LAP. SCN imeanzisha LPNs nchini Lebanon, Jordan[22] na Macedonia[23] Kaskazini pamoja na kusaidia usambamba wake nchini Kenya, CEFs. Kusudi la LPN ni kushirikisha juhudi za P/CVE, kufanya kazi kama shirika kuu la mtaani la kutambua vipaumbele vya mtaani vya P/CVE, kuunda mikakati ya mtaani na kufanikisha shughuli za mtaani za PVE. |
| Makadirio ya Hatari ya Mtaani: Hii inatathmini kuwepo kwa hatari katika mji/eneo la serikali ya mtaa ili kuelewa kinachohitajika kukabiliwa kupitia kwa LAP. Tathmini inaweza kutambua hatari za kutoingilia kati pamoja na kuongeza hatari za kuingilia kati (kuvuruga shughuli, kwa mfano, za vikundi vyenye misimamo mikali na wasajili wao ama wanaowaonea huruma). |
| Kielelezo cha Mantiki: Huu ni mchoro unaoonyesha ToC, kwa kawaida katika muundo wa piramidi, ingawa pia unaweza kuwasilishwa kwa njia changamano zaidi. |
| Mpango Kazi wa Kitaifa (NAP): Huu ni mfumo shirikishi wa kitendakazi wa kitaifa, wa kukabiliana na viongozi wa misimamo mikali ya ghasia yaliyo mazingira mazuri ya ghasia kupitia kwa mtazamo kamilifu, wenye kuhusisha sekta nyingi.[24] |
| Kuzuia/Kukabili Misimamo Mikali ya Ghasia (P/CVE): Ni mbinu nyingi zisizokuwa za kushurutisha, km. ratiba, sera, mikakati ama shughuli zinazopania kupunguza uharamu wa fikra za misimamo mikali ya ghasia ili kuzuia watu ama makundi ya watu kusajiliwa katika misimamo mikali na kuchafuliwa akili na dhana za misimamo mikali kufuata fikra zinazovutiwa na ghasia ili kutimiza malengo ya kijamii, kiuchumi, kidini ama kisiasa.[25] |
| Tathmini Hali: Inarejelea kuelewa muktadha wa ndani na nje wa misimamo mikali (ikiwa pamoja na jinsi wanavyoingiliana) pamoja na wahusika (ikiwa pamoja na miondoko ya kiongozi) na fursa za kukabiliana na suala. Uundaji wa LAP sharti uongozwe na kufahamishwa na matokeo ya tathmini ya hali kama sehemu ya tathmini ya hatari. |
| Hali za Wastani za Kufanya Kazi (SOPs). Mara nyingi hutumiwa kwa kubadilishana na ToR. Istilahi hii inarejelea kazi na majukumu mahsusi ya LPNs ama CEFs, ikiwa pamoja na jinsi wanavyofaa kufanya kazi na kufanya kazi rasmi na mawasiliano. |

| |
|---|
| Maunganiko Thabiti ya Miji (SCN): Maunganiko ya Kimataifa ya mameya, maafisa wa serikali za mitaa na wafanyakazi walio kwenye mstari wa mbele ulioanzishwa na Taasisi ya Midahalo ya Kimikakati (ISD) mwaka wa 2015 katika Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa.[26] |
| Tathmini ya SWOT: Inarejelea tathmini (ama uelewaji bora) wa Uzuri, Unyonge, Fursa na Vitisho vilivyo katika shirika, mkakati au mfumo wa sera – katika hali hii kuunda na kutekeleza LAP. |
| Nadharia ya Mabadiliko (ToC): Inabainisha mchakato sababishi ambao kupitia kwake unatarajia shughuli kuzaa msururu wa mabadiliko yanayoleta matokeo na malengo. Maelezo ya ToC yameundwa ili kwenda pamoja na kielezo cha mantiki na kuangazia kuelezea mahusiano ama mishale baina ya kila kiungo cha mfumo. Maelezo ya ToC yanatafuta dhana zinazobainisha kila unganiko ama mshale katika kielelezo chako cha mantiki, pale panapowezekana kutoa ushahidi unaosaidia kila dai ambalo kiungo kimoja kitasababisha kingine. |
| Masharti ya kufanya kazi (ToR): Hii ni istilahi ambayo mara nyingi hutumika kwa kubadilshana na SOPs. Inabainisha vitekelezwa ambavyo mtu binafsi, muundo, shirika ama muunganiko unafaa kutekeleza ili kuafikia lengo lililotajwa. Inaweza kutumiwa kuelezea kazi na majukumu wazi ya wanachama wa LPN na CEF. |
| Mji-mzima: Huu ni mtazamo ambao hujengwa kwa msingi wa serikali-nzima ama jamii-nzima. Mji-mzima unaashiria kuwa sekta zote za serikali ya mtaa na mashirika ya kijamii yanafanya kazi pamoja ili kuandika na kutekeleza LAP. Vipaumbele vya mji mzima vinazingatiwa ili kuhakikisha kuwa kuna mtazamo kamilifu kwa LPN na CEF. |
| Mpango wa Kila Mwaka wa Kazi: Mpango wa kuelezea shughuli za LAP za mwaka utakaofuata. Mpango wa kazi sharti ujumuishe mazao yanayoleta matokeo ya LAP pamoja na viashiria vya M&E vya kupima shughuli. Mpango kazi sharti pia uonyeshe nani anawajibika kwa kila shughuli na ni wapi ambapo rasilmali zitatoka. Kutokana na hali badilifu ya VE na ufadhili wa muda mfupi, ni mazoea mazuri kwa LAP kuwa na mipango ya kila mwaka ambayo inaweza kusahihishwa mwishoni mwa kila mwaka wa kifedha. |

Yaliyomo —

# Kiambatisho B –
## Aina tatu za kanuni za kuongoza

Kiambatisho hiki kinajumuisha matini nzima kutoka kwa stakbadhi zilizorejelewa katika Sura ya Pili wakati wa kuelezea aina tatu za kanuni za kuongoza. Hii inajumuisha mfano wa kitaifa kutoka Kenya, mfano wa kieneo kutoka LCBC, na mfano wa kimataifa kutoka UNOCT.

| Kanuni Jumuishi | | |
|---|---|---|
| 'Mazao' ya Kenya NSCVE | 'Kanuni Kuu' za LCBC | 'Kanuni Jumuishi' za UNOCT |
| 1 Wakenya kudhihirisha uzalendo | 1 Umiliki wa kitaifa na wa kieneo | 1 Wajibu ni wa nchi wanachama |
| 2 Ukubalifu wa kindani kote nchini Kenya wa njia yetu ya maisha | 2 Uongozi: wa kitaifa, kieneo na kimataifa | 2 Lazima iwe katika mfumo wa UN CT |
| 3 Kuondoa uhalali na kukataliwa kwa fikra za VE | 3 Uwajibikaji wa pamoja | 3 Wajibu wa Umoja wa Mataifa ni kusaidia juhudi za kitaifa |
| 4 Upatikanaji wa onyo ya mapema na zana za kuingilia kati zinazofikika | 4 Ushirikiano na kusaidiana | 4 Washika dau wa sekta nyingi na jumuishi |
| 5 Uwezo wa kusaidia mashirika ya misimamo mikali ya ghasia kuondoa usajili wa wanachama | 5 Ushirikiano wa pamoja wa kutiana nguvu | 5 Sharti iwe na msingi wa ushahidi |
| 6 Athari-lenga, inayoshirikisha na yenye ubunifu | 6 Mitazamo ya mabadiliko kwa uthabiti/maendeleo | 6 Lazima 'isaidie msimamo wa jamii dhidi ya VE' km. kukuza heshima kwa haki za binadamu |
| 7 Msaada wa kuendelea kutoka kwa viongozi wa kitaifa na wa mtaa | 7 Kuheshimu ala haki za binadamu za kieneo, kimabara na kimataifa | 7 Kuchangia SDGs |
| 8 Rasilmali zilizoko kwa michakato ya kujibu-haja | 8 Kujenga uwezo kwa ajili ya kutoa huduma bora. | 8 Kuambatanisha maazimio ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kwa magaidi wapiganaji wa nchi za kigeni (FTFs), wanawake, vijana na sheria ya ndani ya kiutu. |
| 9 Inayoongozwa-na-ushahidi, isiyokuwa na maoni makali, na iliyojengwa kwenye ufahamu unaofaa wa mtaa. | 9 Ujumuishaji wa jinsia zote | 9 Kumbatia mtazamo wa 'kutodhuru yeyote' |

## Masharti ya Utaratibu ama Uongozi

### 'Kuongoza na Kushirikisha CAP' Kenya

1. CAP itaundwa na kamati iliyochaguliwa na kamishna akishauriana na serikali ya kaunti na kujumuisha wawakilishi wa wahusika
2. P/CVE ya Baraza la Kaunti la Ushauriano (CEF) itaundwa. Uwenyekiti wake utakuwa wa pamoja kati ya gavana na kamishna na litahusisha wawakilishi kutoka kwa wahusika.
3. NCTC itakuwa mwanchama wa CEF.
4. CEF watakutana mara kwa mara kulingana na maamuzi yao na pia wataweza kuitisha vikao maalum.
5. CAP watakuwa wa kulenga utendaji na watafuatilia vipaumbele vichache ndani ya kila kipindi cha wakati
6. Utekelezaji wa CAP utatambua na kufuata majukumu ya kiusalama na yasiyo ya kiusalama
7. Sehemu ya utekelezaji wa CAP ya Makundi ya mashirika ya kijamii lazima iwe ya uwazi na uwajibikaji kwa CEF kwa mtendo na matokeo yao
8. Washirika wa utekelezaji wa CAP sharti wadhihirishe sura ya tafaifa kidini, kikabila, kidemografia, kitaaluma, kijamii na kisiasa kadri iwezekanavyo.
9. Mashirika ya Kibinafsi, wafadhili na mashirika yanayotekeleza CAP sharti yajisajili hapa https://citizensupport.go.ke kwa ajili ya kuramanisha juhudi za kitaifa, mafunzo na msaada.
10. Washirika wote wa CAP sharti wajitolee katika kulinda na kuendeleza kwa hali zote katiba ya Kenya, na hasa Mswada wa Haki za Binadamu na kaida zake
11. Wenye kiti wenza wa CEF sharti wahakikishe kuwa ripoti za maendeleo za kila mwaka, mazao na matokeo ya CAP zinachapishwa
12. Sharti CEF izungumze na washirika wa kigeni na wafadhili katika namna iliyo na muundo inayotambua kazi yao ya kidiplomasia na vingine muhimu

| 'Njia za Utekelezaji' za LCBC | 'Kanuni za Kufuatwa na za Kitaasisi' za UNOCT |
|---|---|
| Kanuni 3 za uwajibikaji:<br>1. Matokeo<br>2. Fedha<br>3. Ufanisi<br><br>Mbinu za utekelezaji<br>• Kamati andalizi<br>• Sekritariati<br>• Ushirikiano wa raia na jeshi<br>• Kazi Mipango ya Mipaka | 1. Anzisha<br>2. Kusanya<br>3. Changanua<br>4. Unda<br>5. Tekeleza<br>6. Fuatilia |

| Mihimili ya Mikakati ya Sehemu za Kipaumbele | | |
|---|---|---|
| **'Mihimili ya Kazi ya CVE' ya Kenya** | **'Mihimili ya Kuingilia Kati' ya LCBC** | **'Maeneo Makuu ya Maudhui' ya UNOCT** |
| 1 Mhimili wa kisaikolojia | 1 Ushirikiano wa kisiasa | 1 Mazungumzo na kuzuia migogoro |
| 2 Mhimili wa elimu | 2 Haki za usalama na bindamu | 2 Uongozi bora, haki za binadamu na kuzingatia sheria |
| 3 Mhimili wa kisiasa | 3 Kunyang'anya silaha, kupunguza hamasa, kukarabati hulka, na kuwarejesha watu wanaohusishwa na Boko Haram | 3 Kuzungumza na jamii |
| 4 Mhimili wa usalama | 4 Msaada wa kibinadamu | 4 Kuwezesha vijana |
| 5 Mhimili wa imani na kifikra | 5 Uongozi na kandarasi ya kijamii | 5 Usawa wa kijinsia na kuwezesha wanawake |
| 6 Mhimili wa mafunzo na ujengaji wa uwezo | 6 Urejeshaji na uendelevu wa kijamii, kiuchumi na kimazingira | 6 Elimu, kuendeleza stadi na kufanikisha ajira |
| 7 Mhimili wa sanaa na utamduni | 7 Elimu, mafunzo na stadi | 7 Mawasiliano ya kimkakati, mtandao na mitandao ya kijamii |
| 8 Mhimili wa sheria na sera | 8 Kuzuia misimamo mikali ya ghasia, na kujenga amani | |
| 9 Mhimili wa vyombo vya habari na mitandao | 9 Uwezeshaji wa jinsia na wanawake | |

# Kiambatisho C – Orodha ya kukagua uundaji wa LAP

Serikali za mitaa ama CSOs zinazotengeneza LAP zinaweza kutumia orodha ifuatayo ya kukagua ili kuhakikisha kuwa zimeangazia viungo vyote vya kuunda na kutekeleza LAP.

| Awamu | Hatua | Vitendo | Nani |
|---|---|---|---|
| Anzisha | Pata mkakati wa kuungwa mkono n wanasiasa | ○ Tafuta washika dau wa serikali ambao hawajashirikishwa<br>○ Panga kongamano ama mkutano wa washikadau na serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali<br>○ Jenga maelewano kuhusu haja ya LAP na umuhimu wa P/CVE<br>○ Pata idhinisho kutoka kwa mamlaka ya serikali inayofaa ili kuendelea kuanzisha ukadiriaji wa hatari | ○ Serikali ya mtaa[27]<br>○ CSOs na serikali ya mtaa<br>○ Tawi kuu la serikali ya mtaa |
| | Fanya tathmini ya hatari ya mtaa | ○ Zindua ukadiriaji wa hatari<br>○ Zungumza na mtafiti wa mtaani kufanya ukadiriaji wa hatari<br>○ Tambua hali na kiwango cha hatari za VE ya mtaani<br>○ Elezea jinsi ambavyo waendeshaji wa mtaani wa VE wanaojulikana wanaweza kuongeza viwango vya hatari<br>○ Weka katika kategoria sababu za hatari kulingana na kutoka kwa na kwa: watu binafsi, dhana na taasisi<br>○ Halalisha tathmini ya hatari na washikadau wale wale kutoka kwa kongamano la mwanzo<br>○ Kutokana na makadirio ya hatari, bainisha iwapo LAP inahitajika<br>○ Pata idhini kutoka kwa mamlaka yanayofaa ya serikali ili kuendelea na utungaji wa LAP | ○ Serikali ya mtaa<br>○ Serikali ya mtaa<br>○ Mtafiti<br>○ Mtafiti<br>○ Mtafiti<br>○ CSOs na serikali ya mtaa<br>○ Serikali ya mtaa<br>○ Tawi kuu la serikali ya mtaa |
| | Anzisha jopo kazi la muda | ○ Pata amri rasmi, ama kisawe chake, kuanzisha jopo kazi la muda na wajibu<br>○ Bainisha mwenyekiti/wenyekiti wenza wa jopo kazi la muda<br>○ Tunga ToR inayojumuisha: sheria, taratibu, majukumu na kazi, na rasilmali<br>○ Alika serikali na CSOs kujiunga na jopo kazi la muda<br>○ Andaa mkutano wa mwanzo kuhalalisha ToR na kuweka makataa ya kumaliza nakala | ○ Tawi kuu la serikali ya mtaa<br>○ Serikali ya mtaa<br>○ Serikai ya mtaa<br>○ Serikali ya mtaa<br>○ Jopo kazi la muda |

| Awamu | Hatua | Vitendo | Nani |
| --- | --- | --- | --- |
| Tunga | Fanya tathmini ya hali | ○ Zungumza na watafiti wa mtaani ama wasomi ili kusaidia | ○ Jopo kazi la muda |
| | | ○ Andaa mikutano ili kuainisha washika dau wakuu wa mtaani | ○ Jopo kazi la muda |
| | | ○ Tambua vitisho vya kinyumbani, waendeshaji na walio katika hatari – kwa kujenga juu ya tathmini ya mtaani ya hatari | ○ Jopo kazi la muda na watafiti wa mtaa ama wasomi |
| | | ○ Sahihisha sera, miundo na shughuli ambazo zinaendelea kutekelezwa ambayo inawiana na P/CVE | |
| | | ○ Tambua taasisi za kifedha na rasilmali za kibinadamu zilizoko na zilizo na wajibu kuangazia P/CVE na masuala yote yanayohusika na misimamo mikali, chuki na ugaidi | |
| | | ○ Tambua shughuli za CSO zinazoendelea na zinazosaidia kazi ya serikali inayohusika na P/CVE | |
| | | ○ Tambua mapengo ya kiufundi na uzuri wa wahusika waliopo na wanaofanya kazi inayohusiana na P/CVE | |
| | | ○ Tafiti kuhusu michakato ya mtaani ya mtandaoni na isiyokuwa mtandaoni | |
| | | ○ Tambua walengwa wa LAP | |
| | | ○ Tambua sababu zozote za kisiasa ama kijamii ambazo huenda zikaathiri utendaji wa LAP, ama kichanya au kihasi | |
| | | ○ Tafiti kuhusu mitazamo ya umma kuhusu misimamo mikali na upimaji wa ustahimilivu, ikiwezekana kulingana na demografia na ujirani | |
| | | ○ Fanya tathmini ya muktadha wa kimtaa ya kihistoria, kisiasa, kijamii na kiuchumi kama inavyohusika na P/CVE | |
| | | ○ Wasilisha tathmini ya hali kwa washikadau wa serikali wanaofaa | ○ Serikali ya mtaa na jopo kazi la muda |
| | Andaa ToC | ○ Sahihisha mbinu za M&E, stadi na mifumo ambayo serikali ya kitaifa na serikali ya mtaa hutumia, ikiwa pamoja na NAP iwapo kuna moja iliyoko | ○ Jopo kazi la muda |
| | | ○ Weka lengo wazi la LAP | ○ Jopo kazi la muda |
| | | ○ Andaa matokeo ya kuafikika ya kati na ya wakati huo ya LAP | ○ Jopo kazi la muda |
| | | ○ Tunga maelezo ya ToC ili kuelezea uhusiano kati ya matokeo ya kati na wakati huo na lengo na dhana zozote | ○ Jopo kazi la muda |
| | | ○ Tunga viashiria ili kupima lengo na matokeo | ○ Jopo kazi la muda |
| | | ○ Wasilisha ToC kwa washika dau wa serikali wanaohusika | ○ Serikali ya mtaa na jopo kazi la muda |
| | Fanya mashauriano ya jamii | ○ Tambua makundi makuu ya jamii ya kuzungumza nayo na kuweka makataa ya mazungumzo<br>○ Andaa mkakati wa kuzungumza na hadhira zilizo 'ngumu-kufikia'<br>○ Unda ajenda ya wastani na vipengele vya mjadala vitakavyotumiwa katika mazungumzo yote. Yajumuishe: vipindi vya mafunzo ya P/CVE, kuelezea njia za mabadiliko chanya katika jamii, kuhalalisha tathmini ya hali, kuhalalisha ToC, na kukusanya maoni kuhusu suluhu za kimtaa<br>○ Tengeneza vifaa sahili vya mafunzo katika vipindi vya elimu<br>○ Wasilisha mazungumzo na kuandaa ripoti<br>○ Fanya marekebisho kwa tathmini hali na ToC nchini Kenya.<br>○ Tunga LAP | ○ Jopo kazi la muda<br>○ Jopo kazi la muda<br>○ Jopo kazi la muda<br>○ Wasomi ama wataalamu wa mtaani<br>○ Jopo kazi la muda<br>○ Jopo kazi la muda na watafiti ama wasomi wa mtaani |

| Awamu | Hatua | Vitendo | Nani |
|---|---|---|---|
| Tunga | Anzisha miundo ya ushirikishi | ○ Tambua mashirika ama taasisi wanachama wa LPN<br>○ Karibisha wanachama wa LPN kujiunga na uweke mahali pa anwani<br>○ Bainisha mwenyekiti ama wenyekiti wenza wa LPN<br>○ Tunga ToR ama SOP zinazojumuisha: sheria, taratibu, kazi na majukumu, sheria za kazi, itifaki za kushiriki habari, mikutano kufanyika baada ya muda gani na mbinu za kutoa ripoti<br>○ Itisha mkutano wa mwanzo ili kuhalalisha ToR ama SOP | ○ Jopo kazi la muda<br>○ Serikali ya mtaa<br>○ Serikali ya mtaa<br>○ Serikali ya mtaa<br>○ Serikali ya mtaa |
| | Halalisha na kuunda sheria | ○ Halalisha LAP, kupitia kwa kongamano ama misururu ya mazungumzo<br>○ Pitisha sheria ya mtaa ama amri kuu kuhalalisha LAP | ○ Serikali ya mtaa<br>○ Tawi kuu ama la bunge la serikali ya mtaa |
| Tekeleza | Andaa hafla ya uzinduzi | ○ Tambua mahali panapofaa pa kufanyia mkutano wa hafla ya uzinduzi<br>○ Alika washika dau kutoka sekta nyingi<br>○ Tengeneza nakala za LAP, huenda ukataka kuchapisha nakala ya mwanzo<br>○ Pata wawasilishaji na utunge ajenda | ○ Serikali ya mtaa<br>○ Serikali ya mtaa na LPN<br>○ Serikali ya mtaa<br>○ Serikali ya mtaa na LPN |
| | Toa habari kuhusu LAP | ○ Tengeneza mpango wa mwaka mmoja wa mawasiliano<br>○ Tekeleza mpango wa mawasiliano<br>○ Mwishoni mwa mwaka rejelea mawasiliano na kusaili iwapo ufahamu wa jamii wa LAP na yaliyomo umeongezeka | ○ LPN<br>○ LPN<br>○ LPN |
| | Tengeneza mpango kazi wa mwaka | ○ Sahihisha ToC na kuulizana maswali kuhusu mazao yanayotekelezeka na shughuli zinazosaidia kupata matokeo<br>○ Zungumza na wataalamu wa awali wa jamii ili kupata maoni, ama fanya mazungumzo zaidi<br>○ Andaa kazi mpango, ukionyesha mashirika ama taasisi za kuwajibikia kila shughuli<br>○ Halalisha kazi mpango na washika dau husika<br>○ Chapisha kazi mpango | ○ LPN<br>○ LPN<br>○ LPN<br>○ LPN, CSOs na serikali ya mtaa<br>○ Serikali ya mtaa |
| | Fadhili mpango kazi wa mwaka | ○ Hakikisha kuwa kuna ufadhili kwa kila shughuli katika kazi mpango ukitumia mbinu nne tofauti za ufadhili: kutumia kikamilifu rasilmali zilizopo, kutumia fedha za mtaa na za serikali kuu, kutafuta msaada kutoka kwa sekta ya kibinafsi na kufikia fedha za wafadhili ama CSO. | ○ LPN na serikali ya mtaa |
| | Tambua sera za ziada za kusaidia LAP | ○ Sahihisha orodha ya makala ya mapengo katika sera katika LAP<br>○ Himiza uundaji wa sera mpya, kubadilisha zile zilizoko ama kutekeleza sera zilizopo | ○ LPN na CSOs |

| Awamu | Hatua | Vitendo | Nani |
|---|---|---|---|
| Fuatilia | Tathmini athari | ○ Weka pamoja M&E zote na maelezo ya mabadiliko<br>○ Wasilisha matokeo kwa serikali ya mtaa na jamii<br>○ Jumuisha mafunzo yaliyopatikana katika LAP na kazi mpango ya mwaka ufuatao | ○ LPN<br>○ LPN na serikali ya mtaa<br>○ LPN |
| | Tengeneza mpango mpya wa kazi wa mwaka | ○ Sahihisha tathmini ya athari ili kuelewa shughuli gani zilifanikiwa, na kama kuna zozote ambazo hazikutekelezwa, na kwa nini<br>○ Ulizana maswali kuhusu mazao mapya na shughuli<br>○ Yape mahirika ama taasisi shughuli na viashiria vya tungo<br>○ Halalisha kazi mpango na washika dau husika<br>○ Chapisha kazi mpango | ○ LPN<br>○ LPN<br>○ LPN<br>○ LPN, CSOs na serikali ya mtaa<br>○ Serikali ya mtaa |
| | Sahihisha miundo ya ushirikishi | ○ Sahihisha na kurekebisha LPN ToR ama SOP kama inahitajika<br>○ Sahihisha uanachama wa LPN ili kuongeza ama kuondoa mashirika ama taasisi ama kurekebisha anwani | ○ Uongozi wa LPN<br>○ Uongozi wa LPN |
| | Rekebisha tathmini ya hatari ya mtaa [28] | ○ Sahihisha na kurekebisha tathmini ya hatari ama anzisha mpya<br>○ Kutegemea tathmini ya hatari iliyosahihishwa, bainisha iwapo LAP inatakikana | ○ Serikali ya mtaa<br>○ Serikali ya mtaa |
| | Rekebisha LAP[29] | ○ Bainisha kiwango ambacho stakbadhi iliyorekebishwa inatakikana<br>○ Tunga ToR ili kutathmini LAP na kuzungumza na mtafiti wa mtaani, msomi ama shirika ili kusaidia<br>○ Fanya utafiti wote wa tathmini ya LAP<br>○ Halalisha tathmini ya LAP na jamii.<br>○ Tunga LAP iliyorekebishwa<br>○ Halalisha LAP iliyorekebishwa<br>○ Zindua LAP iliyorekebishwa | ○ LPN<br>○ LPN<br>○ Mtafiti ama msomi<br>○ LPN<br>○ LPN<br>○ Serikali ya mtaa<br>○ Serikali ya mtaa |

# Kiambatisho D –
## Kiwiliwili cha LAP

Kifuatacho ni kiolezo ama kiwiliwili ambacho serikali za mitaa na CSOs zinaweza kutumia wakati wa kutunga LAP zao. Hiki kinanuia kuwa mwongozo na kimetengenezwa ili kufaa muktadha wako. Mifano ya LAPs kutoka kote duniani inaweza kupatikana kwenye SCN Resource Hub.

### Dibaji

LAP sharti ianze na **dibaji kutoka kwa kiongozi wa serikali ya mtaa** – kama vile meya, gavana ama kiongozi mkuu. Dibaji hii itaonyesha kwamba LAP inaungwa mkono na uongozi mkuu wa serikali yako ya mtaa na itaongeza uhalali katika stakbadhi yako.

### Muhtarasi

Huku ikiwa kwamba LAP nzima lazima iandikwe kwa lugha nzuri, washikadau wengi hawatakuwa na wakati ama kuona haja ya kusoma stakbadhi yote. Kwa hiyo, **kurasa kama 1-2 za muhtasari** utaweza kutoa ujumbe muhimu zaidi. Muhtasari sharti ujumuishe sehemu zinazoonyesha umuhimu wa LAP, utoe kwa ufupi kile ambacho LAP inanuia kuafikia, na iwe na maelezo mafupi kuhusu jitihada za kutekeleza.

### Utangulizi

Utangulizi sharti uanze kwa **kutoa muktadha na kwa nini kuwe na LAP**. Huenda ukataka kuonyesa sheria za mtaani na zile za kitaifa, sera ama mikakati ambayo LAP imefaidika kutokana nayo. Ni sharti pia ujumuishe maelezo mafupi ya uundaji wa jopo kazi la muda na amri kuu zozote ama sheria ambazo ziliaanzisha LAP kirasmi.

Utangulizi sharti pia ujumuishe **sehemu ya mbinu** ambayo inatoa maelezo kuhusu jinsi ambavyo jopo kazi la muda na watafiti wa mtaa na wasomi walifanya tathmini ya hatari, tathmini ya hali na mazungumzo na jamii.

### Maelezo mafupi kuhusu misimamo mikali ya ghasia, kukingamiza na migogoro

Anwani ya sehemu hii sharti ibadilishwe ili itumie istilahi faafu ya muktadha kulingana na masuala ambayo LAP yako inaangazia. Sehemu hii inategemea pakubwa kwa **tathmini hali** ili kutoa picha ya muktadha wa misimamo mikali ya ghasia na mada nyingine yoyote inayofaa. Tathmini hali yenyewe sharti iwe stakbadhi ndefu, kwa hiyo sharti uhakikishe kuwa unawasilisha taarifa muhimu zaidi wa njia wazi zaidi kwa makusudi ya LAP.

### Mipaka na Lengo

Sehemu hii sharti ianze kwa **kubainisha kanuni zinazoongoza** ambazo LAP yako itatumia katika utekelezaji wake. Kumbuka kuwa kuna makundi matatu ya kanuni zinazoongoza. Vigezo jumuishi vinavyobaini mkakati na barabara ya LAP, mchakato na uongozi, vyote vitalazimisha mbinu gani inayofaa kutumika katika kutunga LAP na muundo wa ushirikishi, na maeneo ya kipaumbele (wakati mwingine huitwa mihimili) huainisha kategoria pana za maudhui ya kuingilia kati.

Ni sharti sehemu hii **ionyeshe ToC**, kuelezea lengo na matokeo ya kati na yale ya papo kwa hapo. Lazima pia uelezee namna ambavyo matokeo yatasaidia katika kuafikia lengo na dhana zozote zilizoko.

Kujenga kwenye misingi ya ToC, sehemu hii sharti basi ionyeshe **matokeo yanayotarajiwa kwa kila eneo la kipaumbele** – hivi ni kusema kuwa, kwa kila sehemu ya maudhui ama mhimili uliochaguliwa kwa LAP.

## Kutekeleza LAP

Inapendekezwa kuwa LAP ijumuishe shughuli mahsusi na mazao kuainishwa kwa kindani katika mpango wa kazi wa kila mwaka. Hata hivyo, sehemu hii sharti ionyeshe katika njia pana **hatua tofauti zilizochukuliwa, kuingilia kati na shughuli** zinazotarajiwa kufanyika ili kuafikia matokeo. Huenda ukahitajika kupanga haya kwa mujibu wa sehemu za kipaumbele.

Sehemu hii basi ni lazima ielezee **jinsi ambavyo utelekezwaji** wa LAP utashirikishwa – hivi ni kusema kuwa, kupitia kwa LPN na kamati ya sekta nyingi. Nchini Kenya, hii inaitwa CEF. Orodha ya uanachama ya ToR ama SOP ya LPN sharti iwe stakbadhi tofauti; hata hivyo, lazima ueleze kwa njia pana namna LPN itakavyofanya kazi na aina ya washika dau wanaounda uanachama.

Sehemu hii lazima basi **ielezee hatua za uwajibakaji** ambazo zinachuliwa ili kufaulisha LAP pamoja na LPN. Kama ilivyo katika sehemu iliyotangulia, maelezo ya haya yatakuwa katika ToR ama SOP; hata hivyo, LAP lazima itoe muhtasari wa laini ya juu.

Sehemu hii sharti pia ielezee jinsi ambavyo LPN na serikali ya mtaa inapanga **kutathmini athari** ya LAP na kujumuisha makataa muhimu ya marekebisho pamoja na muundo wa marekebisho. Kama ilivyotajwa katika chombo hiki cha zana, imependekezwa kuwa tathmini zote pamoja na viashiria viambatanishwe mara moja kwa mwaka ili athari iweze kuchunguzwa kabla ya kutungwa kwa kazi mpango ya mwaka unaofuata.


## Uendelevu

Uendelevu ni kiungo muhimu cha LAP na sharti kijuimuishe katika stakbadhi nzima. Hata hivyo, sehemu hii inaweza kuongeza vitu kama vile **vianzo vikuu vya ufadhili.** Sehemu hii inaweza pia kutagusana na sera zilizopo, mikakati, ama mipango ya maendeleo ambayo shughuli za LAP zinaweza kupania kujumuishwa nazo.

# Kiambatisho E – Kiolezo cha kazi mpango ya mwaka

| Shughuli | Mazao | Tokeo/Matokeo faafu ya papo hapo | Tokeo/Matokeo Faafau ya Kati | Shirika linalowajibikia Utekelezaji[30] | Washikadau Wengine | Makataa | Rasimali Zinazohitajika[31] | Rasilmali Zilizopo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |

# Kiambatisho F – Kiolezo cha ToC



# Kiambatisho G – Kiolezo cha Jedwali la Kiashiria cha Kufuatilia

| Kiwango cha kuingilia kati/ Matokeo | Nambari Ya kiashiria | Kiashiria | Ufafanuzi wa kiashiria | Chanzo cha deta/ Kutenganisha | Chanzo cha deta | Mzunguko wa ukusanyaji | Kuripoti | Msingi | Mwisho | Lengo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| LENGO | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| Tokea la Kati 1: | 1 | | | | | | | | | |
| | 2 | | | | | | | | | |
| Tokea la Kati 2: | 1 | | | | | | | | | |
| | 2 | | | | | | | | | |
| Tokea la Kati 3: | 1 | | | | | | | | | |
| | 2 | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| Tokea la Kati 1: | 1 | | | | | | | | | |
| | 2 | | | | | | | | | |
| Tokea la Kati 2: | 1 | | | | | | | | | |
| | 2 | | | | | | | | | |
| Tokea la Kati 3: | 1 | | | | | | | | | |
| | 2 | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| Zao 1: | 1 | | | | | | | | | |
| | 2 | | | | | | | | | |
| Zao 2: | 1 | | | | | | | | | |
| | 2 | | | | | | | | | |
| Zao 3: | 1 | | | | | | | | | |
| | 2 | | | | | | | | | |

# Makala ya tamati

[1] United Nations, Department of Economic and Social Affairs, "68% of the world population projected to live in urban areas by 2050, says UN", tarehe 16 mwezi wa tano 2018. Inapatikana mtandaoni kwenye: https://www.un.org/development/desa/en/news/population/2018-revision-of-world-urbanization-prospects.html

[2] Kwa makusudi ya chombo hiki cha zana, istilahi 'miji' inarejelea miundo yote ya serikali z mitaa kama vile kaunti, majimbo, mikoa ama manispaa.

[3] Sterman, D. and Rosenblatt, N., All Jihad is Local Volume II: ISIS in North Africa and the Arabian Peninsula, New America, 2018. Inaptikana mtandaoni kwenye: https://d1y8sb8igg2f8e.cloudfront.net/documents/All_Jihad_Local_Vol2.pdf

[4] United Nations Development Programme, Journey to Extremism in Africa: Drivers, Incentives and the Tipping Point for Recruitment, 2017. Inaptikana mtandaoni kwenye: https://www.undp.org/content/dam/denmark/docs/Journey%20to%20Extremism_report.pdf

[5] Global Counterterrorism Forum (GCTF), Memorandum on Good Practices on Strengthening National-Local Cooperation in Preventing and Countering Violent Extremism Conducive to Terrorism, 2020 Inaptikana mtandaoni kwenye: https://www.thegctf.org/Portals/1/Documents/Framework%20Documents/2020/GCTF%20Memorandum%20on%20Good%20Practices%20on%20Strengthening%20NLC%20in%20PCVE.pdf?ver=2020-09-29-100315-357

[6] Feve, S. and Dews, D. National Strategies to Prevent and Counter Violent Extremism: An Independent Review, Global Center on Cooperative Security, 2019. Inaptikana mtandaoni kwenye: https://www.globalcenter.org/wp-content/uploads/2019/10/GCCS-2019-National-Strategies-Prevent-Counter-Violent-Extremism-Independent-Review.pdf

[7] Pkalya, D. "Kenyan Stakeholders Call for Implementation of Local Action Plans to Stem Youth Radicalisation and Extremism", Strong Cites Network (SCN), tarehe 15 Januari 2021. Inaptikana mtandaoni kwenye: https://strongcitiesnetwork.org/en/kenyan-stakeholders-call-for-implementation-of-local-action-plans-to-stem-youth-radicalisation-and-extremism/

[8] Institute for Strategic Dialogue (ISD), Assessment of Kwale, Nakuru and Isiolo County Action Plans (CAPs), 2021. (haijachapishwa kufikia wakati wa kuchapisha chombo hiki cha zana).

[9] European Forum for Urban Security (EFUS), Prevention of Radicalization Leading to Violent Extremism: Methodological guide for the development of a local strategy, 2017. Inaptikana mtandaoni kwenye: https://issuu.com/efus/docs/publication_liaise2_en

[10] National Counter Terrorism Centre (NCTC), Guide to Developing County Action Plans, 2018.

[11] Inarejelea uchanganuzi ama uelewaji bora wa Ubora, Unyonge, Fursa na Hatari katika shirika, mkakati ama muundo wa sera.

[12] Dukic, S., Hulse, T. and Hooton, D., Community Resilience Study: Kumanovo, North Macedonia, Institute for Strategic Dialogue (ISD), 2021.

[13] EFUS (2017), uk. 33.

[14] Prevention Institute & Urban Networks to Increase Thriving Youth Unity through Violence Prevention, Multi-Sector Partnerships for Preventing Violence: A Collaboration Multiplier Guide, 2014. Inaptikana mtandaoni kwenye: https://www.preventioninstitute.org/sites/default/files/uploads/Multi-Sector%20Partnerships%20for%20Preventing%20Violence%20Part%203.pdf

[15] Table of outcome syntax modified from Global Affairs Canada (GAC), Results-Based Management for International Assistance Programming at Global Affairs Canada: A How-to Guide, second edition, 2016.

[16] Ibid.

[17] Ibid.

[18] Uchanganuzi wa yliyomo ni mbinu ya utafiti ambayo kupitia kwayo matini ama njia zingine zinachanganuliwa katika viwango vya kupimika, kama vile mara ngapi neno ama maudhui yametumika. Uchunguzi maalum unaweza utumia ala kama vile uchunguzi wa mahitaji ama uchunguzi wa hatari.

[19] Kusek, J. & Rist, R., Ten Steps to a Results Based Monitoring and Evaluation System, World Bank, 2004.

[20] Ujsiri wa ufahamu ni kipimo kilicho cha mapendeleo na kinarejelea mtazamo wa mtu binafsi kuhusu kile anachojua kinyume na kile ambacho anajua kwa kweli. Mara nyingi ujasiri wa ufahamu unapimwa kupitia viwango vya aina ya Likert.

[21] GCTF (2020).

[22] Strong Cities Network (SCN), "SCN in Lebanon and Jordan – 6 Prevention Networks established", 17 July 2017. Inaptikana mtandaoni kwenye: https://strongcitiesnetwork.org/en/scn-lebanon-jordan-6-prevention-networks-established/

[23] Dogani, B. & Joy-Zein, N. "SCN's Local Prevention Network Model expands to the Western Balkans", Strong Cities Network (SCN), tarehe 9 Oktoba 2019. Inaptikana mtandaoni kwenye: https://strongcitiesnetwork.org/en/lpn-model-expands-to-the-western-balkans/

[24] United Nations Office of Counter-terrorism (UNCCT), Reference Guide: Developing National and Regional Action Plans to Prevent Violent Extremism, 1st Edition, 2018. Inaptikana mtandaoni kwenye: https://www.un.org/counterterrorism/ctitf/sites/www.un.org.counterterrorism.ctitf/files/UNOCT_PVEReferenceGuide_FINAL.pdf

Yaliyomo —

[25] Imeazimwa kutoka Government of Kenya, National Strategy to Counter Violent Extremism, NCTC, 2016. Pia angalia Hedaya & Search For Common Ground (SCFG), Countering Violent Extremism: An Introductory Guide to Concepts, Programming, and Best Practices, MENA Edition, 2019.

[26] Kwa taarifa zaidi kuhusu Strong Cities Network (SCN), tazama https://strongcitiesnetwork.org/en/

[27] Kwa makusudi ya chombo hiki cha zana, istilahi 'CSOs' inajumuisha mashirika ya haki, mashinani, na jamii, dini, wanawake na viongozi wa vijana, miongoni mwa wengine.

[28] Iwapo tu mji wako hauna LAP.

[29] Marekebisho ya stakbadhi yafanyike kila mwaka. Hata hivyo, uhuishi wa kindani waweza kufanyika kila unapohitajika na iwapo rasilmali zinaruhusu.

[30] Kwa makusudi ya kiolezo hiki, 'shirika' linajumuisha idara za serikali na zisizikuwa za kiserikali, mashirika ama taasisi.

[31] Rasilmali zinajumuisha za kifedha, kibibinadamu, mitandao, michango, bajeti za serikali ama hazina na aina yoyote ya rasilamali zinazohitajika na kutwaliwa.

ISD Powering solutions to extremism and polarisation

STRONG CITIES